# Nipashe

Jumamosi Juni 12, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580609

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US


**Walimu** jela miaka 112 wizi mtihani

UKURASA 4



**Askari** 34,000 wa Polisi, Magereza wapandishwa vyeo

UKURASA 4



**Dayna amlewesha Davido kimahaba**

UKURASA 11

## SIKU 19 MWANZA

# Kauli 5 za Chalamila

• **Samia** amtumbua usiku mnene, akabidhi ofisi kimya kimya...

*Endelea ukurasa 2*



## Benki, TPSF waona nuru bajeti ijayo

UKURASA 3



## Vigogo taasisi nne waingia matatani

UKURASA 2

**MICHEZO** **WATUNISHA MISULI KUSHINDANA OKT.** UK.23

**MAONI, KATUNI** UK.6

HABARI KITAIFA

# Vigogo taasisi nne matatani

**Na Romana Mallya,** DODOMA

BUNGE limeishauri serikali kuzichukulia hatua taasisi zake nne ili kutilia nguvu masharti ya ukaguzi wa umma.

Taasisi hizo ni Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH), Taasisi ya Tiba ya Mifupa na Mishipa ya Fahamu (MOI), Kampuni ya Mbolea (TFC) na Shirika la Magazeti ya Serikali (TSN).

Spika wa Bunge, Job Ndugai, aliyasema hayo juzi bungeni jijini Dodoma wakati akisoma uamuzi wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) uliofikiwa baada ya kuzihoji taasisi hizo.

Kamati hiyo iliyahoji mashirika 11 ya serikali ambayo hayakuwasilisha hesabu zake ili zikaguliwe na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka 2019/20.

Akisoma uamuzi huo, Spika Ndugai alisema: "Maana taasisi zingine zinajua zitapata hati chafu, kwa hiyo zinakwepa wakati wa ukaguzi na wanapeleka hesabu zao baada ya ukaguzi, mbinu hii tumeigundua na tumestuka kama wana busara wajirekebishe."

Alisema kamati imeishauri serikali kuchukua hatua kwa taasisi hizo ili kutilia nguvu Sheria ya Ukaguzi wa Umma.

Akizungumzia kuhusu TFC na TSN, Spika Ndugai alisema ushauri wa Bunge baada ya kushindwa kufunga mahesabu yake, ni serikali ifanye tathmini ya kina ili kubaini iwapo mashirika hayo yanatakiwa kuendelea kufanya kazi chini ya mfumo wa sasa au kuyafanyia marekebisho makubwa.

Kwa upande wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), kutofunga hesabu kwa sababu ya kutokuwapo kwa makubaliano ya maandishi kati ya mfuko na serikali wa ulipaji wa mkopo wa Sh. bilioni 231, alisema wanaishauri serikali na mfuko huo wakamilishe makubaliano ya kimaandishi ikiwamo ratiba maalum ya upimaji na kuanza kulipa madeni husika kwa ratiba waliyokubaliana.

Kwa upande wa MOI, alisema kutokamilisha mahesabu kutokana na changamoto za mfumo wa kitabibu kutowasiliana ipasavyo na mfumo wa hesabu, wameishauri serikali ifanye uchunguzi wa mchakato mzima wa ununuzi na usimikaji wa mfumo wa shughuli za kitabibu uliopo katika taasisi hiyo.

Alisema lengo ni kubaini kama taratibu zilifuatwa na mfumo huo unamanufaa kwa taifa na kuishauri serikali ipeleke wataalamu wenye sifa ili kufanya ukaguzi na uhasibu kwa sababu imeonekana kuna shida ya sifa za wahasibu.

Spika Ndugai alisema kutokana na kutokamilika kwa wakati kwa taasisi za TANESCO, Shirika la Mawasiliano la Taifa (TTCL) na Shirika la Posta, ushauri wao kwa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi iboreshe mipango ya ukaguzi na kuzingatia ipasavyo wakati wote wa ukaguzi.

Kuhusu kuongezwa kwa muda wa ukaguzi kwa taasisi tatu zikiwamo, Soko la Bidhaa (TMX), Shirika la Reli (TRC) na Mfuko wa Uwekezaji wa Pamoja (UTT), wanaishauri Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi izingatie kwa ukamilifu masharti ya kifungu cha 32 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma.

Alisema ni lazima wawe wanafunga hesabu kwa wakati ili taarifa ya CAG inapopelekwa bungeni iwe na taarifa zao.




Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Selemani Jafo (kushoto), akitoa zawadi kwa Mshauri wa kampuni ya City Engineer Ltd, Moses Mboya, aliyeshiriki kudhamini Mkutano Mkuu wa Tatu wa Mwaka wa wataalam wa Mazingira (TEEA), jijini Dar es Salaam jana. Wa pili kushoto ni Mwenyekiti wa TEEA, Prof. Hussein Sosovele. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Kauli 5 za Chalamila Mwanza

**Na Richard Makore, MWANZA**

ALIYEKUWA Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Albert Chalamila, ameingia katika rekodi ya wakuu wa mikoa waliokaa siku chache katika nafasi hiyo baada ya uteuzi wake kutenguliwa usiku wa manani.

Chalamila 'ametumbuliwa' akiwa ameakaa ofisini kwa siku 19 tangu alipohamishwa kituo cha kazi na Rais Samia Suluhu Hassan Mei 19 mwaka huu.

Kabla ya kuhamishiwa Mwanza, Chalamila alikuwa Mkuu wa Mkoa wa Mbeya.

Taarifa iliyotolewa na Kurugenzi ya Mawasilino ya Rais, Ikulu majira ya 7:40 usiku wa kuamkia jana, ilisema Rais Samia ametengua uteuzi wa Chalamila. Taarifa hiyo haikubainisha sababu za kuchukuliwa kwa uamuzi huo.

Siku tano baada ya kuhamishiwa Mwanza, Chalamila alikabidhiwa ofisi na mtangulizi wake ambaye kwa sasa ni Mkuu wa Mkoa wa Arusha, John Mongella.

Chalamiala aliingia ofisini Mei 24 mwaka huu na kuikalia kwa takribani siku 19 mpaka jana alipokabidhi ofisi kwa mteule mpya.

Baada ya kukabidhiwa ofisi, Chalamila alianza kutekeleza majukumu yake mapya mkoani Mwanza na siku hiyo alikutana na viongozi mbalimbali mkoani humo.

Miongoni mwa viongozi hao ni wakuu wa wilaya, wakurugenzi wa halmashauri, kamati ya ulinzi na usalama, wakuu wa taasisi za umma, viongozi wa dini na wafanyabiashara.

KAULI 5 AKIWA MWANZA

Baada ya kukabidhiwa ofisi mkoani Mwanza, Chalamila alisema kwa takribani miezi miwili tangu kutokea kifo cha Dk. John Magufuli, hakupata usingizi.

Chalamila alisema alikosa usingizi katika kipindi hicho kwa sababu hakujua hatima yake ikiwamo kuendelea kushika nafasi yake kama mkuu wa mkoa.

"Sikupata usingizi kwa takribani miezi miwili, usiku nilikuwa nikilala naacha redio inaongea na niliposikia sauti ya Rais Samia nilishtuka sana," alisema Chalamila siku alipokabidhiwa ofisi mkoani Mwanza.

Kauli yake nyingine ni ya kuwataka wakazi wa Mwanza kunywa bia kwa sababu unywaji pombe unachangia kukuza uchumi.

Chalamila alitoa kauli nyingine kwamba wananchi wanaruhusiwa kuandika mabango ya aina yoyote ikiwamo yenye ujumbe wa matusi wakati akitangaza ziara ya ujio wa Rais Samia mkoani Mwanza.

Kauli hiyo ilionekana kuwa mwiba kwake na hata akachukua hatua Jumatano kuwaita waandishi wa habari na kujaribu kukanusha suala hilo.

Chalamila pia alisema Mamlaka ya Mapato (TRA) ianze kuwaminya kidogo wafanyabiashara wanaokaidi kulipa kodi kwa hiari.

Alisema serikali imetoa mwongozo kwa TRA kwamba ikusanye kodi bila kutumia nguvu, lakini Chalamila akasema lazima kuwaminya kidogo wafanyabiashara wakaidi.

Kauli nyingine aliyotoa Chalamila baada ya kutua Mwanza ni pale aliposema atakuwa mtu wa kwanza kupima kipimo cha CT Scan katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Mwanza ya Sekou Toure.

Alikuwa akizungumzia umuhimu wa wananchi wa Mkoa wa Mwanza kukata bima ya afya ili waweze kupata matibabu bure na kwamba serikali ya Rais Samia imeweka kipimo hicho kwa gharama ya Sh. bilioni mbili.

Chalamila alisema atakuwa wa kwanza kwenda kupima japo haimaanishi kwamba yeye ni mgonjwa.

Katika mazungumzo yake na wananchi siku hiyo, kiongozi huyo pia alizungumzia kifo cha Dk. Magufuli, akiwataka wananchi wa Mkoa wa Mwanza kutoendelea kuhuzunika kwao kunajenga taswira mbaya kana kwamba viongozi walioko madarakani kwa sasa, ndiyo waliohusika na kifo cha kiongozi huyo ilhali siyo kweli.

TAHADHARI YA SAMIA

Wakati akiwaapisha viongozi mbalimbali aliowateua hivi karibuni, Rais Samia alidokeza kile alichokiita 'kibiriti na petroli' alipowalinganisha viongozi wawili wakuu mkoani Mwanza, yaani Chalamila na Katibu Tawala wake, Samike Ngusa.

Rais Samia aliweka wazi tahadhari yake kwa viongozi hao na wengine kwamba timu yake inawafuatilia.

Jana, Chalamila alikabidhi ofisi kwa Mkuu wa Mkoa mpya, Robert Gabriel.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Ofisi ya Habari mkoani Mwanza, viongozi hao walikabidhiana ofisi kimya kimya bila kushuhudiwa na watu wengi.

Gabrieli anachukua nafasi hiyo akitokea mkoani Mara alikokuwa akihudumu kama Mkuu wa Mkoa.

HABARI KITAIFA

# Benki, sekta binafsi waichambua bajeti

**Na Romana Mallya,** DODOMA

WABUNGE, sekta binafsi na taasisi za fedha wameichambua bajeti inayopendekezwa na serikali kwa mwaka ujao wa fedha, wakibainisha inatoa tumaini jipya kwa Watanzania kutokana na kupunguza mzigo wa tozo na kujikita katika maendeleo ya biashara na uwekezaji.

Muda mfupi baada ya Waziri wa Wizara ya Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, kuwasilisha bungeni juzi mapendekezo ya bajeti hiyo, wadau hao walisema ni bajeti inayogusa wananchi moja kwa moja.

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Sekta Binafsi (TPSF), Francis Nanai, alisema kwa kiasi kikubwa imejibu hoja na matamanio ya sekta binafsi kwa kusaidia sekta ya kilimo kwa kuongeza tija na uzalishaji, kuongeza thamani na viwanda ambavyo vitatumia bidhaa za ndani.

"Lengo ni kuongeza tija ya uzalishaji na kuuza bidhaa zetu, bajeti hii imepunguza tozo nyingi kwa lengo la kusaidia maendeleo ya biashara na uwekezaji," alisema.

Nanai alisema anaiona ni bajeti ya kurudisha uchumi ambao utaendeshwa kwa biashara na uwekezaji kwa kiasi kikubwa na imetimiza adhma ya Rais katika hilo.

"Kilichobaki ni kuangalia kile kitabu cha sheria kinasema nini ili kukamilisha tulichokisikia leo (juzi) hapa bungeni," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa CRDB na Mwenyekiti wa Chama cha Sekta ya Benki nchini, Abdulmajid Nsekela, alisema bajeti hiyo imejikita kujenga mazingira mazuri ya sekta binafsi na kufanya kuwapo kwa usimamizi wa miradi mikubwa ya maendeleo.

"Nikiangalia usimamizi wa kuanzia kwenye ngazi ya chini kwa maana tarafa, madiwani kunawezesha kufanya kazi zao vizuri.

"Maeneo mengi bajeti hii imeondoa kodi ili kuleta tija na chachu na kulinda viwanda vya ndani.

"Ni bajeti yenye mwelekeo mzuri na kuweka mazingira ya sekta binafsi kuwa mazuri zaidi," alisifu.

WABUNGE

Mbunge wa Babati Vijijini, Daniel Silo, alisema bajeti hiyo italeta matumaini makubwa kwa kuwa imelenga watu wa sekta tofauti wakiwamo wakulima, wafugaji, wafanyakazi na wafanyabiashara.

Mbunge wa Viti Maalum (CHADEMA), Esther Matiko, akichambua bajeti hiyo alisema baadhi ya maeneo yanatia matumaini na mengine yanatakiwa kufanyiwa kazi ili yakae vizuri. Kuhusu madiwani kulipwa kila mwezi posho ya Sh. 100,000 kutoka serikali kuu, mbunge huyo alisema ni hatua nzuri ya kuweka uwiano na usawa na kukosoa mchanganuo wa ulipaji wa watu hao kwa daraja A walipwe na halmashauri zao.

"Nitaishauri serikali kuwe na malipo yanayofanana kwa daraja A na wale wa madaraja ya chini serikali kuu iwalipe kila mwezi, daraja A kulipwa na halmashauri bado wataendelea kuwa wanyenyekevu kwa wakurugenzi," alisema.

Aliipongeza serikali kwa kusikiliza kilio cha bodaboda kwa kupunguza faini zao za barabarani kutoka Sh. 30,000 hadi Sh. 10,000 na kukosoa ongezeko la ushuru wa matairi ambalo anaona litawaumiza.

Akizungumzia kuhusu tozo ya petroli na dizeli, mbunge huyo alisema zitaongeza gharama za usafirishaji wa mazao na endapo fedha zitakazokusanywa hazitakwenda kufanya kazi zinazotakiwa, tozo hizo zitamuumiza mwananchi.

Kuhusu tozo ya laini za simu ya Sh. 10 hadi Sh. 200 kwa siku, mbunge huyo alisema kwa Mtanzania anayeishi kijijini kwao itakuwa na tatizo.

Hata hivyo, alisema bajeti hiyo kwa ujumla imemtazama mwananchi kwa jicho pana na endapo wataboresha makusanyo ya mapato na kuyaelekeza kwenye miradi ya maendeleo nchi itapiga hatua kiuchumi.

"Ukiangalia fedha inayotoka kwa washirika Sh. trilioni 2.9 tukiweza kujielekeza kwenye maeneo ya kimkakati utalii, usafirishaji, madini, kilimo, mifugo na viwanda hizo Sh. trilioni 2.9 tutaweza kuzikusanya kama nchi na kuacha kuwa tegemezi," alisema.

# Mtanzania wa kwanza kupanda Everest anena

**Na Godfrey Mushi, HAI**

MSICHANA wa kwanza mdogo kwa umri kutoka Bara la Afrika, Rawan Dakik (20), ambaye ameweka rekodi ya kupanda kilele cha Mlima Everest, amewasili nchini baada ya kutimiza ndoto zake hizo.

Vilevile, kijana huyo ameishauri serikali kutambua vipaji vingi zaidi vya vijana, kuvithamini, kuvitangaza na kuviendeleza kwa kuwa mafanikio ya vipaji hivyo yanaliletea taifa heshima.

Rawan aliwasili nchini jana saa 12:47 asubuhi kwenye Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA) akitokea Nepal.

Hadi sasa, Rawal amepanda milima mikubwa sita duniani iliyoko katika mabara sita ambayo ni Kilimanjaro wenye urefu wa mita 5,895, Elbras ulioko Urusi (mita 5,648), Aconcagua wa Argentina (mita 6,961), Carstenz Pyramid wa Indonesia (mita 4,884), Vinson Massif wa Antarctica (mita 4, 8920 na Mlima Everest ulioko Nepal (mita 8,848).

Akizungumza baada ya kupokewa na Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mary Masanja, maofisa wa Bodi ya Utalii Tanzania (TTB) na wahifadhi kutoka Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA), Rawan alisema ushindi wake akiwa msichana mdogo kutoka Afrika na Tanzania anautoa kama zawadi kwa Rais Samia Suluhu Hasan na Watanzania wote ili iwe chachu ya kutambua vipaji vya vijana. "Nimepitia matatizo mengi na hatari nyingi katika safari yangu ya kupanda Mlima Everest, lakini kilichonipa nguvu ni kuona kuwa niliahidi kubeba wajibu wa kulipa taifa langu (Tanzania) heshima, kwa kuweka historia ya kufika kilele cha mlima mrefu zaidi duniani nikiwa msichana wa kwanza mdogo kwa umri kutoka Bara la Afrika.

"Nimekuwa nikifanya mazoezi saa 20 kwa wiki, kwa lengo la kunipa uwezo wa kubeba mzigo wenye kilogramu 35 na kuvuta mwingine wenye vifaa vya kupandia mlima vyenye uzito wa kilogramu 30.

"Nilielekezwa nifanye mazoezi ya kuhimili kupanda mlima Everest ambao ni mkubwa kuliko yote duniani katika hali ya hewa ya chini ya kiwango cha baridi cha nyuzi joto 30, na ikanilazimu kupanda mlima wenye baridi kali wa Kazbek wenye urefu wa mita 5,033 uliopo Georgia nchini Urusi," alifafanua.

Rawan, ambaye ni mkazi wa Jiji la Arusha, Mei 23, mwaka huu saa 9:35 usiku kwa saa za Afrika ya Mashariki, alipeperusha bendera ya Tanzania kwenye kilele cha Mlima Everest.

Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mary, alisema serikali itamwalika rasmi Rawal bungeni jijini Dodoma ili wabunge wamtambue na kueleza matamanio yake kuhusu ukuaji wa sekta ya utalii.




# Mwanataaluma nguli mwenyekiti mpya CBE



**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan amemteua Prof.. Eleuther Mwangeni (pichani) kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Uongozi ya Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) kuanzia Juni 8, mwaka huu.

Prof. Mwangeni ambaye ni mwanataaluma mbobezi, kwa sasa ni Profesa katika Chuo Kikuu cha Ardhi (ARU) na anachukua nafasi ya Prof. Esther Ishengoma ambaye amemaliza muda wake.

Taarifa iliyotolewa na Wizara ya Viwanda na Biashara jana ilisema kutokana na uteuzi wa Mwenyekiti wa Bodi,, Waziri wa Viwanda na Biashara, Prof.. Kitila Mkumbo, ameteua wajumbe sita wa bodi hiyo.

Uteuzi wa bodi hiyo, taarifa ilisema ni kwa mujibu wa Sheria ya Chuo cha Elimu ya Biashara ya mwaka 1965 Sura 315 pamoja na marekebisho yake ya mwaka 2020.

Taarifa hiyo iliwataka walioteuliwa kuanzia Juni 9, mwaka huu kuwa ni Dk. Consolatha Deogratias Ishebabi ambaye ni Mkurugenzi wa Maendeleo ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo, Wizara ya Viwanda na Biashara na Dk. Kenneth Hosea ambaye ni Mkurugenzi wa Elimu ya Juu, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Wengine ni Mwema Punzi ambaye ni Wakili wa Serikali Mkuu, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali; Zahoro Muhaji ambaye ni Mjumbe wa Bodi ya Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPS); CPA. Peter Lucas Mwambuja ambaye ni Rais wa Chama cha Wahasibu Tanzania (AA) na Prof. Wineaster Anderson wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.



Ofisa Msimamizi wa Kodi kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Makao Makuu, Joel Lema, akifafanua jambo kwa mfanyabiashara wa Wilaya ya Kasulu, mkoani Kigoma juzi, wakati wa kampeni ya elimu kwa mlipakodi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Walimu jela miaka 112 udanyangifu mitihani

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Geita, imewahukumu walimu wawili kutumikia kifungo cha miaka 112 jela au kulipa faini ya Sh milioni 420 kwa makosa 28 ya udanganyifu uliyofanyika katika mitihani ya kujipima ya darasa la nne katika Shule ya Msingi Kabayole.

Washtakiwa hao ni Justine Augustine (43) ambaye ni mwalimu wa taaluma na Miraji Abdallah (37) ambaye ni Mwalimu Mkuu wa shule hiyo.

Hukumu hiyo imetolewa jana mjini hapa na Hakimu Mkazi Mwandamizi Aloyce Katemana, baada ya upande wa mashtaka kuthibitisha makosa hayo pasipo kuacha shaka yoyote.

Hakimu Katemana alisema mahakama inatoa adhabu kali dhidi ya washtakiwa ili iwe fundisho kwao na kwa walimu wengine wenye tabia ya udanganyifu wa mitihani kama yao.

Alisema upande wa mashtaka ukiongozwa na Wakili wa Serikali, James Pallangyo, ulipeleka mahakamani mashahidi 24 na vilelezo 15 ambavyo vilithibitisha kuwa washtakiwa walitenda makosa hayo.

Pia alisema washtakiwa wakiwa walimu, walikiuka maadili yao kwa kuwafanyia wanafunzi watoro mitihani ya darasa la nne, kitendo ambacho ni kinyume cha sheria.

Hakimu Katemana alisema ameangalia ushahidi wa pande zote na kugundua kuwa upande wa mashtaka umethibitisha makosa yote pasipo kuacha shaka yoyote na pia mahakama hii imewatia hatiani washtakiwa wote kwa pamoja na kuwataka wajitetee ili mahakama hiyo iwapunguzie adhabu.

Washtakiwa hao waliokuwa wakitetewa na Wakili wa Kujitegemea Erick Lutehanga, walijitetea kuwa wana familia zinawategemea na kuomba mahakama hiyo kuwapunguzia adhabu.

Upande wa Jamhuri ukiongozwa na Wakili Pallangyo, ulidai mahakamani kuwa anaomba mahakama hiyo itoe adhabu kali kwa washtakiwa wote wawili ili iwe fundisho kwao na kwa walimu wengine, kwa kuwa makosa waliyoyafanya yanadumaza taaluma nchini.

Hakimu Katemana alisema kitendo walichokifanya washtakiwa hao ni kibaya kwa kuwa kinakiuka maadili ya kazi yao.

"Hivyo wote wawili mtakwenda gerezani miaka 112 au kulipa faini Sh milioni 420 ili iwe fundisho kwenu na kwa watu wengine wenye tabia mbaya kama zenu. Kila kosa moja ni miaka minne na faini kila kosa moja Sh. milioni 15," alisema. Washtakiwa hao walishindwa kulipa faini hiyo na kupelekwa katika gereza la Geita kutumikia kifungo.

Awali, akisoma hati ya mashtaka, Wakili Pallangyo alidai mahakamani kuwa tukio hilo lilitokea kati ya Novemba 20 na 21, 2019 katika Shule ya Msingi Kabayole mkoani Geita.

Washtakiwa wote kwa pamoja waliamuru wanafunzi 28 wa darasa la tano na darasa la sita kuwafanyia mitihani wanafunzi watoro wa darasa la nne kitendo ambacho ni kinyume cha sheria.

# Maofisa, askari 34,000 wapandishwa vyeo

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WIZARA ya Mambo ya Ndani ya Nchi imewapandisha vyeo maofisa, wakaguzi na askari wa Polisi, Magereza, Uhamiajai, Zimamoto na Uokoaji wapatao 34,106.

Hatua hiyo ni utekelezaji wa agizo la Rais Samia Suluhu Hassan, kutaka watumishi wote wanaostahili, wakiwemo maofisa, wakaguzi na askari wa vyombo vya ulinzi na usalama kupandishwa.

Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, George Simbachawene, alibainisha hayo jana jijini Dodoma wakati wa mkutano wake na waandishi wa habari.

"Katika kutekeleza maelekezo ya Rais, tayari wizara imewapandisha vyeo maofisa, wakaguzi na askari wa ngazi mbalimbali 34,106 walıostahili kupandishwa katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2018/19 na 2020/21", alisema Simbachawene.

Alisema katika idadi hiyo, Jeshi la Polisi limewapandisha vyeo maofisa, wakaguzi na askari 26,464 wakiwamo warakibu waandamizi 110 kuwa makamishna wasaidizi. Pia alisema warakibu 110 wamepandishwa na kuwa warakibu waandamizi, warakibu wasaidizi 241 wamepandishwa kuwa warakibu.

Pia alisema wakaguzi 745 wamepandishwa cheo na kuwa warakibu wasaidizi wa polisi, wakaguzi wasaidizi 890 wakaguzi wa polisi na askari 4,148 wamepandishwa vyeo kuwa wakaguzi wasaidizi wa polisi.

Alisema askari wa 20,220 wamepandishwa vyeo mbalimbali kutoka Konstebo kwenda Koplo 13,751, kutoka Koplo kwenda Sajini 5,619, kutoka Sajini kwenda Stafu Sajini ni 800 na kutoka sajini kwenda Sajini Meja ni askari 50.

Kwa upande wa Magereza maofisa, wakaguzi na askari 6,310 wamepandishwa wakiwamo warakibu waandamizi saba kuwa makamishna na wasaidizi na warakibu 14 kuwa warakibu waandamizi. Pia warakibu wasaidizi 102 wamepandishwa kuwa warakibu, wakaguzi 75 warakibu wasaidizi, wakaguzi wasaidizi 69 kuwa wakaguzi.

"Aidha, jumla ya askari magereza 938 wamepandishwa vyeo na kuwa wakaguzi wasaidizi wa Magereza," alisema

Pia askari wa 5,105 wamepandishwa vyeo mbalimbali kutoka Wadres kwenda Koplo ambao ni 2,632, kutoka Koplo kwenda Sajini ni 1,340, kutoka Sajini kwenda Stafu Sajini ni 1,103 na kutoka Stafu Sajini kwenda Meja ni 30.

Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limewapandisha vyeo jumla ya maofisa,wakaguzi na askari 149, kati ya idadi hiyo jumla ya wakaguzi wasaidizi wa Zimamoto na Uokoaji wanne wamepandishwa cheo na kuwa wakaguzi wa Zimamoto na Uokoaji.

Vilevile, askari wa R& F 145 wamepandishwa cheo kutoka Koplo kwenda Sajini.

Kadhalika alisema Idara ya Uhamiaji imewapandisha vyeo maofisa, wakaguzi na askari 1,183 wakiwamo warakibu wasaidizi tisa kuwa makamishna wasaidizi wa Uhamiaji.

HABARI KITAIFA

# Bil. 362/- kuongeza upatikanaji umeme

**Na Ibrahim Joseph,** DODODMA

SERIKALI ya Tanzania imetiliana saini mkataba wa mkopo wenye masharti nafuu na Ufaransa wenye thamani ya Sh. bilioni 361.71 kwa ajili ya kuzalisha Umeme jua nchini.

Mkataba huo wa ULITIWA SAINI jana Jijini hapa kwa serikali ya Tanzania ikiwakilishwa na Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango, Emmanuel Tutuba huku Ufaransa ikiwakilishwa na Mkurugenzi wa Shirika la Maendeleo la Ufaransa (ADF), Stephanie Mouen, na kushuhudiwa na na Balozi wa Ufaransa nchini, Fedrick Clavier.

Akizungumza baada ya kutia saini mkataba huo, Tutuba alisema mkopo huo alibainisha malengo ya mkopo huo ni kujenga mitambo ya kuzalisha umeme wa jua unatarajiwa kuanza Machi, mwakani na kukamilika Macho, 2023.

Mradi huo, alisema utajengwa Shinyanga wilayani Kishapu na mitambo hiyo inatarajiwa kuzalisha Megawati 150 na utajengwa kwa awamu mbili.

Aliongeza kuwa katika awamu ya kwanza, mitambo hiyo itaanza kuzalisha megawati 50 na zilizobaki zitaendelea katika awamu ya pili.

Pia alisema sehemu ya fedha za mkopo huo zitatumika kuboresha na kuimarisha gridi ya taifa kuifanya ya kisasa kujumuisha umeme nishati jadidifu zenye muda maalumu na kupunguza upotevu wa umeme.

Pia Kadhalika alisema AFD ilitoa msaada wa kufanya upembuzi yakinifu wa mradi huo na kuwa Euro 700,000 zimetengwa na Serikali ya Ufaransa kama msaada wa kitaalamu katika mradi huo.

Naye Mkurungenzi Mtendaji wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Dk. Tito Mwinuka, akizungumza kwenye hafla hiyo, alisema nyongeza ya megawati hizo 150 za umeme jua pindi utakapokamilika utawezesha upatikanaji wa umeme katika migodi ya dhahabu iliyopo maeneo hayo.

Dk. Mwinuka alisema mradi huo utasaidia kuongeza umeme wa uhakika katika gridi ya taifa na kuchochea maendeleo ya kijamii na kiuchumi katika mkoa wa Shinyanga na nchi kwa ujumla.

Alibainisha kuwa serikali imeidhinisha mpango wa taifa wa tatu wa maendeleo wa miaka mitano 2021/22-2025/26 wenye maudhui ya kujenga uchumi shindani na viwanda kwa maendeleo ya watu .

Aliongeza kuwa mpango huo unafuata baada ya mpango wa taifa wa pili wa maendeleo wa miaka mitano 2016/17-2020/21 ambao utekelezaji wake unaishia mwezi Juni, mwaka huu. Balozi Ufaransa nchini, Fedrick Clavier, alisema serikali yao imekubali kutoa mkopo huo kwa sababu unalengo la kuisaidia jamii ya mkoa huo.

Clavier alisema nishati ya umeme jua ni nzuri duniani kwa sababu haiharibu mazingira na uwekezaji wake unakuwa na teknolojia rahisi zaidi.



Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango, Emmanuel Tutuba (kushoto), akibadilishana makabrasha na Balozi wa Ufaransa hapa nchini, Fredrick Clavier, jijini Dodoma jana, baada ya kutiliana saini mkataba wa mkopo wenye masharti nafuu wa sh. biloni 361.71 kwa ajili ya mradi wa kuzalisha umeme jua nchini. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Hatima kesi ya Seth yawekwa kiporo

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, imeambiwa na upande wa Jamhuri katika kesi ya Uhujumu Uchumi, inayomkabili Mkurugenzi wa Kampuni ya Kufua Umeme (IPTL), Herbinder Seth, kwamba wamekubaliana na mshtakiwa kujielekeza kwenye barua yake ya Juni 10, mwaka huu, kuhusiana na hatima ya kumaliza au la kesi dhidi yake.

Madai hayo yalitolewa jana na Wakili wa Serikali Mkuu, Martenus Marandu katika mahakama hiyo iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mkuu, Huruma Shaidi.

Marandu alidai kuwa mshtakiwa aliandika barua akitaka kujua kuhusu hatima ya kesi yake, pande zote mbili wamekubaliana kujielekeza kwenye barua ya Seth ya Juni 10,mwaka huu.

"Mheshimiwa Hakimu upande wa Jamhuri bado tunaomba muda mpaka Jumatatu kwa ajili ya kuifanyia kazi barua hiyo. Siku hiyo tutakuja kuitaarifu mahakama yako kwamba tumefikia wapi tulivyokubaliana, " alidai Marandu.

Hakimu Shaidi alikubaliana na ombi la Jamhuri na kuamuru mshtakiwa apelekwe mahabusu mpaka Juni 14,mwaka huu.

Juni 10, mwaka huu, upande wa Jamhuri uliiomba mahakama iwape muda wa kufanya mazungumzo na Seth kwa ajili ya kupata ufafanuzi wa barua alizoandika yeye binafsi kupitia wakili wake na mahakama ilikubali ombi lao.

Awali, Mahakama hiyo ilielezwa kuwa mazungumzo ya makubaliano ya kumaliza kesi ya uhujumu uchumi inayomkabili Seth yanasubiri mwongozo wa Mkurugenzi Mashtaka (DPP).

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Saimon, alidai kuwa mazunguzo ya kesi dhidi ya mshtakiwa (Seth) yanaendelea yalipoishia na wanasubiri muongozo kutoka kwa DPP mpya aliyeteuliwa hivi karibuni na Rais ili kuwasilisha mahakamani hapo.

"Mazungumzo yanaendelea wanasubiri mwongozo wa DPP mpya ya umaliziaji wa mazungumzo yaliyokuwa yameanza," alidai Wankyo.

Awali, Seth na Wakili wa Kujitegemea Joseph Makandege waliwasilisha ombi kwa DPP wakionyesha nia yao ya kutaka kumaliza kesi kwa kukiri makosa yao lakini Mei 6, mwaka huu, wakili huyo aliondoa nia yake ya kufanya makubaliano na DPP akidai kwamba mazungumzo hayo yamechukua muda mrefu kukamilika.

Mbali na Seth na Makandege mshtakiwa mwingine ni mfanyabiashara James Rugemalira ambaye ni Mkurugenzi wa Kampuni ya VIP Engineering, ambao wanadaiwa kutenda makosa hayo katika Jiji la Dar es Salaam na nchi za Afrika Kusini, Kenya na India.

Washtakiwa wanakabiliwa na mashtaka 12 yakiwamo ya utakatishaji fedha, miongoni kula njama, kujihusisha mtandao wa uhalifu, kughushi na kutoa nyaraka za kughushi na kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu, kutakatisha fedha na kusababisha hasara ya Dola za Marekani 22,198,544.60 na Sh 309,461,300,158.27.

Washtakiwa wanadaiwa kati ya Oktoba 18 ,2011 na Machi 19, 2014 jiji Dar es Salaam, walikula njama katika nchi za Afrika Kusini, Kenya na India ya kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu.

Mwanasheria Makandege, anakabiliwa na mashtaka matano likiwamo la kuisababishia serikali hasara ya Dola za Marekani 980,000.



Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wagombea TFF huu si wakati sahihi wa kulalamikia kanuni

**MAJIRA** ya saa 10:00 alasiri leo itakuwa siku ya mwisho kwa wagombea wa nafasi mbalimbali katika uchaguzi mkuu wa Shirikisho la Soka nchini (TFF), kuchukua na kurejesha fomu za kinyan'ganyiro hicho kinachotarajiwa kufanyika jijini Tanga Agosti 7, mwaka huu.

Kwa mujibu wa Mwenyekiti wa Kamati ya Uchaguzi ya TFF, Wakili Kiomoni Kibamba, nafasi zinazowaniwa katika uchaguzi huo ni kiti cha urais na nafasi sita za wajumbe wa kamati ya utendaji, ambapo hadi jana mchana wagombea saba walijitokeza kuchukua fomu za urais na idadi kama hiyo wakichukua kwa upande wa nafasi za wajumbe wa kamati ya utendaji.

Waliochukua fomu hadi sasa katika nafasi ya urais ni nguli na mchambuzi wa soka nchini, Ally Mayay Tembele, aliyewahi kuwa Mwenyekiti wa Klabu ya Yanga, ambaye kwa sasa ni Mbunge wa Jimbo la Kinondoni (CCM), Tarimba Abbas pamoja na Mbunge wa Jimbo la Mwera mjini Zanzibar, Zahor Mohammed Haji, wengine ni Deogratius Mutungi, Evans G. Mgeusa, Oscar Oscar na Rais wa sasa wa TFF anayetetea nafasi yake, Wallace Karia.

Kwa upande wa nafasi ya Kamati ya Utendaji ni Lameck, Nyambaya, Liston Katabazi, Michael Petro, Sandy Mohamed Kimji, Athuman Kingome Kambi, Khalid Abdallah, Mohamed Aden, Osuri Kosuri na Salum Umande Chama.

Hata hivyo, tangu kufunguliwa tu kwa dirisha hilo la kuchukua fomu Juni 8, mwaka huu, baadhi ya watia nia hao waliochukua fomu, walikuwa wakilalamika kuwapo kwa 'rafu mbaya' kutoka kwa Rais anayetetea nafasi yake, Karia, ambapo Zahor alidai kuwa kumekuwa na kizingiti cha kupata 'Endorsement' (dhamana/kudhaminiwa) kutoka kwa mikoa 26, vyama shiriki vitano na klabu 16, ambapo kila anapobisha hodi anaambiwa tayari wameshamdhamini mgombea huyo.

Hoja hiyo ya 'Endorsement' imekuwa kubwa mno lakini kwa kuwakumbusha tu wagombea hicho ni kipengele kilichopo hata katika chaguzi za CAF na FIFA, na mwaka 2019 Rais wa sasa wa Fifa, Gianni Infantino alipita bila kupingwa kwa sababu alidhaminiwa na nchi zote.

Kwa ujumla malalamiko yamekuwa mengi kutoka kwa watia nia hao na zaidi wakidai kanuni za uchaguzi huo si rafiki kwa wagombea wote na zinapaswa kumulikwa huku wakiitaka serikali kuingilia kati uchaguzi huo.

Lakini Nipashe tunatambua kanuni hizo za uchaguzi hazikutungwa sasa na wadau wote walizipitia na kuridhia zipite kabla ya kuidhinishwa na kuanza kutumika, hivyo kwa wagombea uchaguzi TFF kuanza kuzilalamikia kwa sasa ni jambo la kushangaza.

Tunafahamu wagombea wote hawakukurupuka kugombea nafasi hizo TFF, na ni jambo ambalo walikuwa wamejiandaa kwa muda mrefu na kama ndivyo walikuwa wanazifahamu vema kanuni/sheria zote za kuwania nafasi hizo, hivyo kuanza kuzilalamikia kwa sasa inatufikisha kuhusu weledi wao endapo watapata ridhaa ya kuwa viongozi wenye dhamana na soka letu.

Tunayasema hayo kwa kuwa kwa mgombea ambaye hakukurupuka kugombea nafasi hizo, kama aliona kuna matatizo ama udhaifu katika kanuni/sheria hizo za uchaguzi, alipaswa kupendekeza kufanyike mabadiliko mapema na si suala la kuanza kulilia kwa sasa.

Kinachotufikirisha zaidi ni wabunge hao wawili kuwa mstari wa mbele kulalamikia kasoro hizo, wakati wenyewe ni kati ya watu ambao Watanzania wamewaamini na kuwachagua kwenda kufanya maamuzi mazito bungeni hususan kwenye kutunga ama kufanya mabadiliko ya sheria za nchi.

Hivyo, tunachotaka kukiona kwa sasa ni kila mgombea kupambana kwa kutafuta wajumbe wa kuwaunga mkono, na kama hawatachaguliwa, huu si mwisho wa kugombea nafasi hizo, warudi kujipanga na kutafuta wadau wa kuwaunga mkono katika suala zima la kupigania mabadiliko ya kanuni/sheria hizo za uchaguzi ambazo wanaona si rafiki kwa kila mgombea.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Uchaguzi una maana gani?

Na Barnabas Maro

**UCHAGUZI** ni uteuzi wa kitu, mtu au jambo kulingana na vigezo ambavyo watu au mtu alivyojiwekea. Utaratibu wa kuonesha utashi wa kile unachokitaka na kile usichokitaka. Tendo la mtu kuchagua kitu kwa sababu ya sifa fulani nzuri; uteuzi, upigaji kura.

Shirikisho la Mpira wa Miguu (Kandanda), yaani TFF litafanya uchaguzi wa viongozi tarehe 7 Agosti, mwaka huu jijini Tanga. Utakuwa mpambano kati ya viongozi waliopo madarakani na wanaotaka kutwaa madaraka hayo wakiwa na sababu mbalimbali.

Je, kwa nini kuna watu wengi waliotangaza kupambana na viongozi wanaomaliza muda wao na kwa nini hao waliopo wanataka kuendelea? Kuna mambo ambayo hawajakamilisha kwa hiyo wanataka kuyakamilisha ndipo waondoke kwa heshima au ni kutaka kujinufaisha zaidi? Baadhi yao wamebadilika sana kimaumbile tangu walipopata nafasi hizo. Nadhani naeleweka.

Nafurahishwa sana na methali za wahenga wetu. Kwa mfano walisema: "Leo ni yako kesho sio." Maana yake mtu huwa na uhakika kwa wakati alionao bali si wakati ujao. Pia leo ni siku yako lakini kesho ni ya mwenzako.

Kwa hiyo huu ni ushindani kati ya viongozi waliopo na wanaotaka kutwaa nafasi za waliopo. Ni mvutano kati ya wanaotaka kuendelea kuwa madarakani kwa kutaja maendeleo waliyofanya, huku wagombea wapya wakisahihisha mambo waliyofanya wenzao, hasa kuhusu matumizi ya fedha na mambo yaliyowashinda kutekeleza.

Je, wapenda kabumbu wanaridhishwa na viongozi wanaomaliza muda wao sasa au wamechoshwa na uwapo wao madarakani? Je, wanaotaka kuwaondoa wenzao madarakani wana sababu zipi zitakazowaridhisha wapiga kura ili wawachague wao au ni uroho tu wa madaraka? Au ni yale yasemwayo "kupiga pesa"?

Wagombea wa pande zote mbili wanapaswa kutambua kuwa "Leo ni yako kesho sio." Maana yake mtu huwa na hakika na wakati alionao bali sio wakati ujao. Pia leo ni siku yako lakini kesho ni ya mwenzako.

Kwa hali hiyo wapigakura wanapaswa kuwa makini kuwapa kura wagombea wa upande wowote, kwa kuchambua mambo au maendeleo yaliyoletwa na uongozi uliopo na yatakayoahidiwa na wagombea wapya. Ahadi ni deni.

Wapenda kandanda wanataka kuona maendeleo, hasa kwa timu za taifa badala ya TFF kuwa na mambo ya kushangaza kwa kufanya mambo yanayoonekana dhahiri kuzipendelea Yanga na Simba kwa sababu viongozi ni mashabiki au wanachama wa timu hizo kubwa nchini!

Yapo mambo na uamuzi mwingi yaliyofanywa na TFF kwa manufaa ya timu za Simba na Yanga. Hii inasababisha hata waamuzi wa kati na washika vibendera kuyafumbia macho makosa yanayofanywa na timu hizo! Kwa sababu hiyo si ajabu kuona refa akikataa faulo, bao au penalti ya wazi anayofanyiwa mchezaji wa timu hizo endapo anapenda moja ya timu hizo yaani kati ya Simba na Yanga!

Mfano ni mchezo kati ya Namungo na Yanga. Dakika za mwisho Yanga walipata kona na mchezaji wao akapiga mpira uliotua kichwani kwa mshambuliaji mwenzake, naye akausindikiza kwa kichwa mpaka kimiani, lakini mshika kibendera akalikataa bao lile akidai mpira ulitoka kabla ya kurejea uwanjani.

Wakati wote huo hakunyoosha kibendera chake bali alinyoosha baada ya mpiga kichwa wa mwisho kufunga bao! Kwa nini hakunyoosha kibendera chake kama mpira ulitoka kabla ya kurejea uwanjani ila alikataa baada ya wavu wa Namungo kufungwa? Matokeo yake timu hizo zikamaliza mchezo kwa sare ya kutofungana!

Haki ni jambo linalomstahiki mtu. Kitu au jambo ambalo mtu anastahiki kupata; utendaji, ufuataji na utumiaji wa sheria na kanuni katika kutimiza jambo.

Simba na Yanga zinapopambana na timu zingine humu nchini baadhi ya waamuzi hufanya mambo ya ajabu na aibu yanayoonesha upendeleo wa wazi ilhali TFF inaona, lakini hakuna hatua zinazochukuliwa dhidi ya wahusika. Matokeo yake ni Tanzania kutokuwa na waamuzi wanaochezesha mechi za kimataifa nje ya nchi.

Kwa faida ya wasomaji wa safu hii, kuna tofauti kati ya 'stahili' na 'stahiki.' Maana ya 'stahili' ni kitendo cha mtu kuadhibiwa kutokana na jambo baya alilofanya. 'Stahiki' ni kitendo cha mtu kuwa na haki ya kupata kitu fulani kutokana na ufanisi aliopata: Mfano, "Anastahiki kupewa zawadi kwa kazi nzuri aliyofanya," n.k.

**marobarnabas@yahoo.com**
**0784334 096**

## HABARI KITAIFA




Mkurugenzi Mtendaji wa EATV na East Africa Radio, Regina Mengi (kushoto) na mwanzilishi wa Taasisi ya Flaviana Matata, Flaviana Matata, wakisaini mkataba wa ushirikiano wa kampeni za Namthamini. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kiwanda kuunganisha magari kujengwa nchini

**Na Joseph Mwendapole**

UMOJA wa Kampuni za Kutengeneza Magari Afrika (AAAM), umeonyesha nia ya kujenga kiwanda kikubwa cha kuunganisha magari nchini na tayari umeanza mazungumzo na serikali ili kuleta uwekezaji huo.

Viongozi wa kampuni hizo, jana walifanya mazungumzo na Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Uwekezaji, William Ole Nasha, na Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dk. Faustine Ndugulile, kwenye ofisi za Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), Dar es Salaam.

Akizungumza kwenye ofisi za TIC jana, Naibu Waziri Ole Nasha alisema wawekezaji hao wanaomiliki kampuni kubwa za kuunganisha magari, wamevutiwa na mazingira mazuri ya uwekezaji yaliyowekwa na serikali ya awamu ya sita.

Alisema iwapo wawekezaji hao watajenga kiwanda hicho, itakuwa fursa kubwa kwa Watanzania kwa kuwa wananchi wengi hasa vijana, watapata ajira na serikali itaingiza fedha nyingi kupitia kodi.

"Sisi tumewapokea kwa mikono miwili kwa sababu suala la uwekezaji wa ndani na nje ni ajenda kubwa ya serikali ya awamu ya sita. Kama unataka kupanua fursa ya ajira na kodi lazima ufanye kazi kwa karibu na sekta binafsi," alisema Ole Nasha.

Alisema wawekezaji hao wanataka kujenga kiwanda hicho cha kuunganishia magari nchini, hivyo wamekuja kuzungumza na serikali kuona namna ya kufanya uwekezaji huo.

Naibu Waziri alisema serikali itaendelea kuweka mazingira mazuri ya kisera na kisheria kuondoa changamoto zilizokuwapo ili kuendelea kuwavutia wawekezaji wengi zaidi kuja kuwekeza.

"Wawekezaji wameelewa utayari wa serikali katika kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji na ndiyo sababu katika kipindi kifupi sana idadi ya wawekezaji walioonyesha nia ya kuja imekuwa kubwa... Hawa wanaotaka kuwekeza kwenye uunganishaji magari ni wawakilishi wa kampuni kubwa duniani sisi tutawasikiliza," alisema Naibu Waziri Ole Nasha

Naye Mwenyekiti wa Umoja wa Watoa Huduma za Mafuta (ATOGS), Abdulsamad Abdulrahim, ambaye aliambatana na wawekezaji hao alisema wawekezaji hao wameiona Tanzania kama sehemu muafaka kwa uwekezaji wao kutokana na sifa na mazingira mazuri yaliyopo.

Alisema wamevutiwa na sera ya kuifanya Tanzania kuwa nchi ya viwanda na kwamba kitu pekee wanachohitaji ni uhiyari wa serikali kupokea uwekezaji huo kwa kuwapa leseni ya kufanya uwekezaji.

"Kampuni ya Nissan tayari inakampuni hapa Tanzania na wameajiri watu hapa, Kampuni ya Bosch wamefungua kituo hapa nchini juzi juzi, BWM wapo hapa nchini. Pia Toyota wapo kwenye umoja huu pia hivyo hii ni fursa kubwa sana kwa Tanzania kutengeneza ajira kwa vijana wetu ambao wana utaalamu mbalimbali," alisema

# Rais wa Botswana amvuta Bakhresa

**Na Enock Charles**

RAIS wa Botswana, Mokgweetsi Masisi, amekaribisha kampuni za Bakhersa zinazomilikiwa na familia ya Said Salim Bakhresa, kuwekeza nchini mwake.

Baada ya kutembelea kiwanda cha kutengeneza ngano cha Azam kilichoko Buguruni jijini Dar es Salaam jana, Rais huyo alisema ni muhimu kwa nchi za Kiafrika kulea wawekezaji wake ili bara hilo lijitegemee na kuwa na nguvu za kiuchumi kushindana na maeneo mengine duniani.

"Botswana nimeshawakaribisha kabla hamjaja, ninatazamia kiwanda kingine kama hiki kwetu Botswana na ikibidi mjiite hivyo hivyo Azam msibadilishe jina, tunaamini katika uchumi wa sekta binafsi, tunaamini ujuzi wao. "Kuwa na kiwanda kama hiki katika nchi ya Tanzania chenye uwekezaji unaofikia dola milioni 100 ni jambo kubwa la kujivunia, kazi za serikali hasa katika nchi za Afrika na hata serikali yangu ni kulea kampuni kama hii ya Bakhresa ili zishindane na kampuni zingine duniani," alisema. Rais Masisi alisema ushindani wa Afrika unatakiwa kuvuka mipaka na kushindana na nchi zingine duniani ili kuwa imara kiuchumi na hilo litawezekana pale nchi za Kiafrika zitakaposhikana mkono na kuwa sera za pamoja za kiuchumi. Rais Masisi pia alihimiza kampuni binafsi kulipa kodi ya serikali ili kuiwezesha serikali kuwahudumia wananchi wake na pia kujitolea kutoa huduma kwa jamii kwa kuwa bila jamii sekta binafsi haiwezi kuendelea.

Waziri wa Viwanda na Biashara, Profesa Kitila Mkumbo, alisema kiwanda cha ngano cha Bakhresa kinasaidia kuchakata mazao, jambo alisema halifanyiki katika nchi nyingi za Afrika ambazo huzalisha mazao mengi bila kuchakatwa. Mkurugenzi wa Kampuni za Bakhresa, Salim Aziz, alisema familia hiyo inamiliki jumla ya viwanda 20, vikiwamo 17 Tanzania Bara na vitatu Zanzibar.

Alibainisha kuwa kiwanda hicho cha ngano kina uwezo wa kuzalisha tani 2,500 za ngano kwa siku. Aziz alisema bidhaa za kampuni hiyo zinauzwa ndani ya nchi na nje ya nchi kama vile Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Angola, Somalia, Comoro, Falme za Kiarabu, Qatar, Ufilipino na Vietnam.

# Watiwa mbaroni tuhuma za uhalifu

**Na Maulid Mmbaga**

JESHI la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam limekamata watu 10 kwa tuhuma za kujihusisha na uhalifu na kukutwa na vifaa vinavyodaiwa vya wizi.

Miongoni mwa bidhaa wanazodaiwa kukutwa navyo ni gari likiwa na tani moja ya nondo, simu za mkononi, komputa mpakato na viambaza (TV).

Kamanda wa Polisi wa Kanda hiyo, Muliro Muliro, alisema jijini Dar es Salaam jana kuwa baadhi ya watuhumiwa hao walikuwa wakitumia pikipiki kupita mitaani na maeneo yenye hudum za miamala ya pesa na kupora kwenye ofisi hizo au kuvizia wanaochukua pesa na kuwafuatilia nyuma hatimaye kuwapora.

Alisema baadhi ya watuhumiwa wamekuwa wakipokea mali za wizi, kuiba vifaa vya ujenzi kwenye miradi mbalimbali na simu za mkononi 118 zilizoporwa katikati ya jiji, kompyuta mpakato 29, kompyuta mbili kwa ajili kufuta kumbukumbu (flash), viambaza 13 na vifaa vya magari.

"Sambamba na operesheni hii, pia amekamatwa Mohamed Mussa maarufu kama Kibosile, tapeli sugu ambaye amekuwa akighushi nyaraka mbalimbali bandia za serikali na ambazo si za serikali kwa kutumia mihuri mbalimbali na kujipatia pesa kwa njia ya udanganyifu.

"Vitendo hivyo vimekuwa vikichafua taswira ya serikali," alidai na kubainisha kuwa mtuhumiwa huyo alikamatwa na vitu kama vile vyeti vya kuhitimu sekondari, vyeti vya hati za tabia njema za Jeshi la Polisi na vibali vya uraia kwa wageni nchini.

Vifaa vingine ni mihuri 24 ya taasisi za serikali na binafsi kama Wizara ya Mambo ya Nje, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Manispaa ya Ilala, CRDB, NMB, STANBIC BANK, Rita, wanasheria, maofisa watendaji, polisi na idara mbalimbali, kadi za benki mbalimbali 16, skana mbili za kughushi nyaraka, hati za kusafiria 33 za Tanzania na za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC). Kamanda huyo alisema kumekuwapo na wimbi la watu kuibiwa kwa njia ya mtandao ambapo amekamatwa Abdalah Risham na mwenzake wakiwa ni miongoni mwa watuhumiwa wa uhalifu wanaotuma ujumbe kwa namba mbalimbali kwa watu mbalimbali kwa lengo la kuwaibia.

"Katika ufuatiliaji, watuhumiwa hao sugu wamekamatwa na laini 20 za mitandao mbalimbali ya simu pamoja na simu mbili wanazotumia kufanyia uhalifu huo, watuhumiwa wote wanaendelea kuhojiwa na taratibu za mashtaka zikikamilika watapelekwa mahakamani.

"Jeshi la Polisi linatoa onyo kwa wahalifu wote hasa wanaojihusisha na uhalifu wa kutumia silaha za moto kwa sababu kimsingi mazingira ya ukamataji wa mtuhumiwa anayetumia silaha yatalilazimisha jeshi kutosita kutumia silaha wakati wa utekelezaji wa kazi zake hasa ukamataji," alisema.

HABARI KITAIFA

# RC akerwa na uhalifu

**Na Francis Godwin,** IRINGA

MKUU wa Mkoa wa Iringa, Queen Sendiga, ameliagiza Jeshi la Polisi mkoani hapa kupitia polisi kata, kukomesha uhalifu kwenye maeneo yao na kuwa hatavumilia kuendelea kwa vitendo hivyo.

Sendiga alitoa agizo hilo jana kupitia kikao maalum cha baraza la madiwani katika Halmashauri ya Wilaya ya Iringa na kubainisha kwamba amekuwa akisikia malalamiko ya wananchi juu ya uhalifu kwenye mitaa yao jambo linalowanyima amani na usalama wa mali zao.

Kutokana na kushamiri kwa vitendo hivyo, alitaka polisi kata kuwajibika kukomesha matukio ya uhalifu kwenye maeneo yao kwa kushirikiana na madiwani na kamati za ulinzi na usalama za kata na wilaya .

Alisema si vyema wananchi waishi kwa hofu wakati vyombo vya ulinzi na usalama vipo na wajibu wao ni kusimamia ulinzi na usalama.

Sendiga alisema hatavumilia vitendo vya uhalifu kwenye mkoa huo, hivyo yeyote atakayezembea kutimiza wajibu wake atawajibishwa.

Alimwagiza Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Iringa, Juma Bwire, kujipanga na askari wake kufanya misako ya wahalifu ili mkoa uendelee kuwa salama kwa uzalishaji mali na si matukio ya uhalifu.

Pia mkuu huyo wa mkoa aliiagiza Halmashauri ya Wilaya ya Iringa kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Iringa kutatua migogoro ya ardhi ndani ya siku 30 na kama watashindwa wapeleke ofisini kwake.

# Maofisa utumishi waonywa udanganyifu

**Na Veronica Mwafisi,** KONDOA

MAOFISA Utumishi watakaobainika kudanganya kuhusu madai ya malimbikizo ya mishahara ya watumishi kuwa wamewasilisha kwa ajili ya kufanyiwa kazi wakati si kweli, watachukuliwa hatua.

Naibu Waziri, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Deogratius Ndejembi, alisema hayo juzi wakati akizungumza na watumishi wa Halmashauri ya Mji Kondoa na Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa.

Alisema kuna baadhi ya maofisa utumishi hawatekelezi wajibu wao kikamilifu na kusababisha Ofisi ya Rais Utumishi kutupiwa lawama.

Ndejembi aliwaelekeza wakurugenzi kuwasimamia maofisa utumishi ili watekeleze majukumu ipasavyo ikiwamo kushughulikia fomu za madai ya malimbikizo ya watumishi ili yafanyiwe kazi kwa haraka na hatimaye kupunguza malalamiko ambayo yanashusha ari ya watumishi.

"Madai ya watumishi yakichelewa kulipwa, mnasingizia fomu ziko Utumishi wakati si kweli.

Mara nyingi fomu hizi zinakuwa ziko kwenu wakurugenzi kwa sababu maafisa utumishi wenu kujifanya miungu watu,'" alisema.

Ndejembi alisema madai ya watumishi ni haki yao ya msingi kwa kuwa wanatumia jasho lao kulitumikia taifa, hivyo wanastahili kulipwa na si hisani.

Kuhusu upandishwaji madaraja kwa watumishi, Ndejembi amewaelekeza maofisa utumishi nchini kuhakikisha wanatenda haki kwa wanaostahili kupandishwa madaraja kama Rais Samia Suhuhu Hassan alivyoelekeza.

"Tujitume kwa bidii tusimwangushe Rais ambaye ameonyesha nia thabiti ya kuwajali watumishi wa umma katika kulinda maslahi na hak i zao za msingi," alisisitiza.

Ndejembi pia aliwataka maofisa utumishi kuwa makini katika mchakato wa kuwapandisha madaraja watumishi wanaostahili kupanda na kuongeza kuwa yeyote atakayebainika kusababisha mtumishi kutopata haki hiyo atachukuliwa hatua.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Kondoa, Sezaria Makota, alimshukuru Ndejembi kwa kufika wilayani hapa kuzungumza na watumishi na kusisitiza uwajibikaji kwa watumishi hao.

Alisema hapendezwi kuwapo kwa madai ya malimbikizo ya mishahara na ya upandishwaji vyeo ambayo hayajafanyiwa kazi na maofisa utumishi katika wilaya yake na kuongeza kuwa hatasita kuwachukulia hatua watakaoshindwa kutekeleza maelekezo.



Ofisa Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), Mhandisi Cyprian Luhemeja, akizungumza na waandishi wa habari jana baada ya kuwashwa kwa mtambo wa maji Ruvu Chini, kufuatia kukamilika kazi ya marekebisho ya bomba la zenge la inchi 48 eneo la Victoria mkoani Dar es Salaam. Kupasuka kwa bomba hilo kulipelekea ukosefu wa huduma kwa wananchi wa Bagamoyo hadi Kigamboni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wapewa mafunzo ubora wa kuhifadhi nafaka

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

MAWAKALA wa Forodha na wafanyabiashara wa mahindi na nafaka zingine, wamepatiwa mafunzo kuwajengea uelewa kuhusu sumukuvu, visababishi, madhara yake na namna ya kuhifadhi mazao.

Maeneo hayo ni kuhusu taratibu za kupata ushauri wa kitaalamu wakati wa kusafirisha shehena nje ya nchi, taarifa za fursa za masoko na upatikanaji wa taarifa pamoja na taratibu za kupata vibali vya kusafirisha mazao nje ya nchi.

Mafunzo hayo yalitolewa kwa siku tatu kuanzia Juni 7, mwaka huu, na Shirika la Viwango Tanzania (TBS) katika mipaka iliyoko Kanda ya Kaskazini ambayo ni Horohoro-Tanga, Holili - Kilimanjaro na Namanga-Arusha.

Lengo ni kuwawezesha mawakala wa forodha na wafanyabiashara kuondokana na changamoto za shehena zao kukataliwa na nchi walizokuwa wakipeleka biashara zao.

"Mawakala wa forodha na wafanyabiashara wa mahindi na nafaka walikuwa wakikabiliana na changamoto ya shehena zao kukataliwa kuingia kwenye nchi wanakopeleka kwa sababu ya kuwa hafifu.

Hii inatokana na ukweli kwamba hawakuwa na taarifa yoyote ya maabara inayoonesha shehena zao zilipimwa na kukidhi viwango na hiyo ilipelekea baadhi ya wafanyabiashara hao kupata hasara," alisema Ofisa Masoko wa TBS, Rhoda Mayugu wakati akizungumzia lengo la mafunzo hayo. Alisema wafanyabiashara na mawakala wa forodha wanatakiwa kuhakikisha mahindi na nafaka wanazonunua zimeandaliwa katika hali ya usafi, lakini pia zichambuliwe na zile zilizooza, zenye uvundo na zilizonyauka ambazo hata kwa macho zikiangaliwa huonekana kuwa dhaifu.

Kwa mujibu wa Mayugu, wanapoona dalili hizo waelewe kwamba uwezekano wa kuwa na sumukuvu ni mkubwa zaidi na kusisitiza kwamba lazima waelewe kuwa sumukuvu haionekani kwa macho, bali kwa vipimo vya maabara.

"Iwapo mahindi au nafaka zingine zitabainika kuwa na sumukuvu madhara yanaweza kutokea kwa watumiaji yakiwamo ya kiafya au ya kiuchumi," alisema Mayugu.

Alisema kiafya yapo madhara ya muda mfupi ambayo ni kuumwa tumbo, manjano, kutapika na degedege, huku madhara ya muda mrefu yakiwa ni kansa ya ini, kupungua kwa kinga mwilini, udumavu wa watoto na hata kupoteza maisha.

Ofisa huyo alisema wafanyabiashara na mawakala wa forodha wanatakiwa kutumia msaada wa kitaalam unaotolewa na TBS wakati wa usafirishaji wa shehena nje ya nchi.

Kupitia utaratibu huo, alisema TBS itachukua sampuli kutoka katika shehena iliyotayari kusafirishwa na sampuli hiyo itapimwa kwenye maabara na mteja atapewa ripoti ya majibu ya maabara atakayoitumia wakati wa usafirishaji.

Alisema ripoti hiyo itamsaidia kusafirisha shehena yake bila usumbufu na vikwazo vyovyote.

HABARI DODOMA



# Kiama chaja wanaonyanyasa wazee

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, amesema serikali haitasita kuwachukulia hatua wale wote watakaobainika kuendelea kuwafanyia vitendo vya ukatili wazee.

Dk. Gwajima aliyasema hayo jijini hapa jana, wakati akitoa tamko kwa waandishi wa habari kuhusu kuelekea maadhimisho ya kimataifa ya kupinga ukatili dhidi ya wazee Juni 15, yenye kaulimbiu `Tupaze Sauti Kupinga Ukatili Dhidi ya Wazee´.

Alisema katika kuhakikisha usalama wa wazee nchini, serikali inaratibu utekelezaji wa Mkakati wa Kitaifa wa Kutokomeza Mauaji ya Wazee wa mwaka 2018/19 -2022/23 na kwamba sita imejizatiti kuona wazee wanafurahia uzee wao katika taifa.

Watu hao, alisema wanapaswa kufahamu kuwa mkono wa sheria ni mrefu na ni suala la muda tu kama si leo basi kesho utawafikia na sheria itachukua mkondo wake kikamilifu.

"Wakumbuke kuwa hata wao watazeeka na hata wanayofanyia wengine wao watafanyiwa maana nguvu ya kuzuia mabaya inatokana na umoja wa jamii katika kuyakataa mabaya dhidi ya wengine," alisema.

Awali, alisema Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012 inaonyesha kuwa wazee walikuwa 2,507,568 kati ya hao wanawake ni 1,307,358 na wanaume ni 1,200,210.

Alifafanua kwa mujibu wa sensa hiyo, wazee ni asilimia 5.6 ya Watanzania wote 44,928,923 na asilimia 80 wanaishi vijijini.

Pia alisema Ripoti ya Taifa ya Makadirio ya Watu ya mwaka 2013-2035 kwa mwaka 2020/21 inaonyesha kuwa Tanzania inakadiriwa kuwa na wazee 2,524,559 wakiwamo wanaume ni 1,205,619 na wanawake 1,318,940.

Aidha, Sera ya Taifa ya Wazee ya mwaka 2003 inatambua kuwa wazee ni hazina ya taifa kutokana na ujuzi na uzoefu walionao katika masuala mbalimbali ya kiuchumi na kijamii.

Dk. Gwajima alisisitiza kuwa sera hiyo pia imetoa mwongozo wa kuhakikisha wazee wanatambuliwa na kupewa fursa ya kushiriki shughuli za kila siku za maendeleo yao na taifa kwa ujumla.

Alisema katika kuhakikisha hazina hii inatumika ipasavyo, serikali inaendelea na uundaji wa mabaraza ya wazee kote nchini na kwamba mabaraza 14,883 yameundwa kuanzia ngazi za vijiji/mitaa, kata, wilaya na mikoa.

Kwa mujibu wa Waziri, lengo la serikali ni kuhakikisha mabaraza ya wazee yanaundwa katika ngazi zote ili kuhakikisha wanashirikishwa ipasavyo katika maendeleo ya taifa na yanatumika kama chombo cha kuelimisha wazee kuhusu ulinzi na usalama wao.




Kaimu Mkuu wa Utawala wa Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), Kanali Hassan Mabena akizungumza na waandishi wa habari katika Makao Makuu Jeshi hilo, jijini Dodoma, kuhusu kuongezwa vijana wa kidato cha sita kujiunga na JKT. **PICHA: RENATHA MSUNGU**

# Ataka elimu kuhusu akiba chakula

**Na Peter Mkwavila,** KONGWA

SERIKALI imeshauriwa kutoa elimu stahiki kwa wakulima namna ya kutunza akiba ya chakula badala ya kuuza au kutengenezea pombe.

Naibu Katibu Mkuu wa Kanisa la PHAM Tanzania, Askofu Julias Bundala, alisema hayo jana alipokuwa akizungumza na waumini wa kanisa hilo wilayani Kongwa.

Alisema janga la corona limesababisha uchumi wa mataifa mengi kuathirika, ikiwamo Tanzania, hivyo kuwapo kwa uhaba wa chakula. Kutokana na hali hiyo, alisema serikali inatakiwa kutoa elimu hiyo kwa wakulima ili wajiwekee akiba ya kutosha.

Kiongozi huyo alisema Watanzania ambao wako katika mikoa ambayo inazalisha chakula kwa wingi, wanatakiwa kutunza chakula badala ya kukiuza mapema kwa bei ya kutupa au kutengenezea pombe.

"Ni utamaduni uliojengeka kuwa kuelekea kipindi hiki cha mwezi wa kuanzia Juni hadi Agosti, kumekuwa kukifanywa shughuli nyingi za kuwapeleka watoto jando, kuoa na kuolewa na kwa kipindi hicho chakula kingi hutumika.

"Nitoe ushauri kwa serikali itumie wataalamu wake kuwaelimisha wakulima, ili atambue madhara ya kuuza chakula mapema na matumizi ambayo siyo stahiki kama kupika pombe na kufanya sherehe ambazo si za lazima," alisema.

Aliwashauri wakulima katika maeneo yao ambayo hawakupata mavuno wanunue chakula na kuweka akiba zaidi.

Mwangalizi wa Kanisa la PHAM Tanzania Jimbo la Kongwa, Chimaisi Isaya, aliomba wilaya hiyo kupiga marufuku sherehe ambazo hazina tija ambazo zinatumia nafaka na kusababisha njaa.

Alisema kuwa kutokana na hali ya hewa kutokuwa mzuri na kuwapo dalili za uhaba wa mavuno ya kutosha ya chakula ni wajibu wa wakulima kutunza chakula walichonacho ili kuepukana na tabia ya kuomba serikalini.

"Kuna tabia ya watu ambao wanatumia chakula vibaya wanauza ovyo na wengine kutengeneza sherehe ambazo hazina tija na pindi wanapoishiwa wanaanza kuwa ombaomba jambo ambalo ni aibu,"alisema.

## JKT yaongeza vijana mafunzo

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

JESHI la Kujenga Taifa (JKT) limeongeza idadi ya vijana waliohitimu kidato cha sita kwa ajili ya kujiunga na mafunzo kwa mujibu wa sheria kwa mwaka 2021.

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa JKT, Brigedia Jenerali Rajab Mabele, Kaimu Mkuu wa Utawala wa JKT, Kanali Hassan Mabena, alisema jeshi hilo lilipanga kuchukua vijana 35,000 lakini hadi sasa limeita vijana 40,000.

Kanali Mabena alisema vijana hao ambao hawajaripoti mpaka sasa, wanatakiwa kuripoti katika kambi ya kuhudhuria mafunzo ya JKT kwa mujibu wa sheria kwa mwaka 2021.

Alisema jeshi hilo limeongeza majina ya vijana kwenda kuungana na wenzao walioitwa hapo awali katika mafunzo hayo.

Kanali Mabena alisema walitarajia kuwaita vijana 35,000 lakini waliotwa mpaka sasa jumla yao ni 40,000 huku akisisitiza kuwa mafunzo hayo yataendeshwa kwa muda wa miezi mitatu tu.

"Naomba kusisitiza hapa mafunzo ya vijana hawa kwa mwaka huu ni miezi mitatu tu na si mwaka mmoja kama ambavyo inasemwa. Huko mitaani kuna watu wanasema mafunzo ni mwaka mmoja, hii si kweli," alisema na kuongeza:

"Maneno hayo yamesababisha baadhi ya vijana kukata tamaa ya kuhudhuria mafunzo. Kimsingi upo mpango wa kuongeza muda hadi kufikia mwaka mmoja lakini suala hilo bado lipo kwenye majadiliano, hivyo kwa mwaka huu mafunzo ni miezi mitatu kama kawaida."

Alisema vijana walioitwa awali na bado hawajaripoti pamoja na walioitwa awamu hii ya pili, wanatakiwa kuripoti kwenye kambi za JKT walizopangiwa mara moja na mwisho ni Juni 17, mwaka huu.

Aidha, Kanali Mabena alisema wahitimu wenye ulemavu wa kuonekana kwa macho waripoti katika kambi ya Ruvu, Mlandizi mkoani Pwani ambayo ina miundombinu ya kuhudumia makundi hayo.







Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale Zanzibar, Lela Mohammed Mussa, akifungua mkutano wa wafanyabiashara na watendaji wa Benki ya Equity, wenye lengo la kuelezea fursa zinazopatikana katika benki hiyo, Unguja juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mwinyi aahidi mapambano zaidi dhidi ya corona kunusuru uchumi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema uchumi wa Zanzibar umeathirika kutokana na janga la corona na kueleza kuwa serikali imejipanga kukabiliana na ugonjwa huo.

Dk. Mwinyi alisema hayo Ikulu jijini Zanzibar, alipozungumza na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Dunia, Kanda ya Afrika, Dk. Taufila Nyamadzabo.

Alisema pamoja na kuwa suala la afya kutokuwa la Muungano, serikali inasubiri mapendekezo ya kamati ya kitaifa iliyoundwa hivi karibuni na Rais Samia Suluhu Hassan ili kuona njia bora ya kukabiliana na ugonjwa huo.

Aliiomba Benki ya Dunia kuendelea kuisaidia Zanzibar kupitia nyanja mbalimbali ili kukuza uchumi wake.

Dk. Mwinyi alizitaja sekta za uchumi wa buluu na utalii kuwa ziko katika mipango ya serikali ili kufanikisha azma ya kuinua uchumi wa Zanzibar.

Aidha, aliipongeza Benki ya Dunia kwa ushirikiano na misaada inayoipatia Zanzibar na kuiwezesha kufanikisha miradi mbalimbali ya maendeleo.

Naye Dk. Nyamadzabo alisema Benki ya Dunia itaendeleza ushirikiano wake na Zanzibar pamoja na kuzipatia misaada mbalimbali nchi wanachama.

Aliyataja maeneo ambayo Benki ya Dunia imeweka kipaumbele kuwa ni kuzisaidia nchi wanachama, ikiwamo Zanzibar katika kipindi hiki kuwa ni pamoja na kuwajengea uwezo watendaji, kuimarisha mifumo ya ajira na ya fedha.

Dk. Nyamadzabo pia alisema Benki ya Dunia itaendelea kufanyakazi kwa karibu na nchi wanachama katika masuala mbalimbali.

# 'Acheni kuandika habari kuumiza watoto'

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAANDISHI wa habari wametakiwa kulinda haki na utu wa watoto wanapoandika habari za watoto waliodhalilishwa kijinsia ili kutowaumiza na kuwadhalilisha.

Hayo yalisemwa juzi na Mhariri Mkuu wa Cloud Media Group, Joyce Shebe, wakati akiwasilisha mada kuhusu uandishi wa habari za watoto katika mafunzo kwa waandishi wa habari kuhusu siku ya Mtoto wa Afrika mafunzo ambayo yaliandaliwa na shirika la kimafunzo kwa wandishi wa habari la Internews, kupitia njia ya mtandao (zoom).

Alisema ni lazima waandishi wa habari kuzingatia usalama wa watoto, hivyo ni vyema kufuata sheria na maadili ya uandishi wa habari ili kutowaletea madhara wanaporipoti taarifa zao.

Shebe aliwataka waandishi hao kuhakikisha wanatoa elimu kwa jamii kupitia sauti na kalamu zao katika kulinda haki za mtoto ikiwamo elimu na kulindwa na vitendo vyote vya ukatili na udhalilishaji.

Alisema vyombo vya habari vina nafasi kubwa ya kuitengeneza jamii ya sasa ili hapo baadaye kuwe na viongozi wenye maadili na wanaojitambua.

"Ni kweli hata ukiona baadhi ya vyombo vya habari vinakwenda kijijini ujue wanafuatilia habari za watoto waliotelekezwa, waliobakwa au kufanyiwa ukatili. Lakini mazuri wanayoyafanya hayaandikwi kwa upana," alisema.

Naye Mkurugenzi Maendeleo ya Jamii Tanzania, Sebastian Katiku, alisema bado vyombo vya habari hawajazipa umuhimu mkubwa habari za watoto na kusababisha wakati mwengine kuripotiwa wanapofanyiwa ukatili au udhalilishaji.

"Vyombo vya habari vilivyo vingi vina madawati ya michezo, mazingira na wanawake ingawa bado upatikanaji wa madawati kwa watoto ni mdogo," alisema.

Alisema mafunzo hayo yalioandaliwa na Internews kwa waandishi wa habari yanaweza kuwa mwanga na kupata mawazo wa kihabari ya kuandika habari hizo.

Akifunga mafunzo hayo, Mwandishi Mkufunzi kutoka Internews, Alakoko Mayombo, alisema mafunzo hayo kwa waandishi wa habari yawe mwanzo mzuri kwao katika kuibua habari za watoto.

Alisema wakati umefika sasa waandishi wa habari wakaliona kundi hilo kwa kuandika habari au kutengeneza vipindi vinavyogusa haki zao kama yalivyo makundi mengine.

"Internews inawategemea mno ninyi waandishi na wanaharakati wengine. Sasa muwe mabalozi wema kwa kuchambua na kutetea haki za watoto,' alisema.

# Wiki msaada wa sheria kuanza leo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

ZANZIBAR kwa mara ya pili inaadhimisha Wiki ya Huduma ya Msaada wa Kisheria na maadhimisho hayo yanafanyika leo mgeni rasmi ni Makamu wa Kwanza wa Rais Zanzibar, Othman Masoud Othman.

Akizungumza jana na waandishi wa habari kuhusu maadhimisho hayo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, Haroun Ali Suleiman, alisema bado kuna wimbi kubwa la wananchi wanakabiliwa na changamoto mbalimbali zinazohitaji msaada zaidi wa kisheria.

Haroun alisema serikali kwa kushirikiana na wadau, wameamua kuwafikia wananchi wa mijini na vijijini kwa kuwapa elimu ili kupata msaada wa kisheria na kuwatatulia chagamoto zinazowakabili.

"Katika jamii yetu bado watu wengi hawana elimu lakini pia wanakabiliwa na changamoto mbalimbali za kisheria, hivyo serikali kwa kushirikiana na Shirika la Msaada wa Kisheria (LSF), tumeamua kutumia Wiki ya Msaada wa Kisheria kuwafikia wananchi hao Unguja na Pemba," alisema.

Waziri Haroun aliwaomba wadau mbalimbali wa maendeleo kushirikiana na serikali katika kuhakikisha wananchi wanatatuliwa changamoto mbalimbali za kisheria hususani wanawake.

"Nataka kuwaomba wadau mbalimbali kuungana na serikali katika kuwatatulia wananchi changamoto za kisheria hususani wanawake na watoto ambao ndio wahanga wakubwa wa udhalilishaji", alieleza.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa LSF, Lulu Ng'wanakilala, alisema shirika hilo linaendelea kuwa wafadhili wakubwa katika shughuli mbalimbali na huduma za upatikanaji wa haki nchini.

Alisema kwa LSF inaona faraja kubwa kuendelea kuwa wafadhili wa maadhimisho hayo kwa mwaka huu ambapo inatokana na makubaliano ya miaka mitatu waliyoingia na Wizara ya Katiba na Sheria. "Kupitia uwezeshaji wa kisheria LSF tumekuwa tukifanya kazi ya kukuza upatikanaji wa haki kwa wananchi wote hasa wanawake kwa kutoa ruzuku katika mashirika takribani 200 yanayotoa huduma za msaada wa kisheria na wasaidizi wa kisheria zaidi ya 200 nchi nzima" alisema.

Mkurugenzi wa Idara ya Msaada wa Kisheria, Hanifa Ramadhani Said, alisema huduma za msaada wa kisheria zinazotolewa na watoa huduma za msaada wa kisheria ni pamoja na ushauri wa kisheria na msaada wa uwakilishi mahakamani.

Alisema kwa mwaka 2019/2020 watoa huduma wa kisheria wamewafikia wananchi 122,149 wakiwamo wanawake 63,834, wanaume 54,334, watoto wa kiume 3,029 na watoto wa kike 952 katika maeneo mbalimbali ya Unguja na Pemba



**AKON KWELI WEWE KIDUME** Uk.14

JUMAMOSI JUNI 12, 2021

Nipashe MWANGA WA JAMII

BT BURUDANI TELE



KAROGEKA

# Dayna amlewesha Davido kimahaba?

HIVI karibuni mwanamuziki wa kike wa Bongo Fleva, Dayna Nyange, ameachia ngoma kali ambayo amemshirikisha mkali kutoka Nigeria, Davido.

Ngoma hiyo inayoitwa 'Elo', pamoja na kuleta msisimko kwa mashabiki, lakini kumeibua mashaka ukaribu uliopo kati ya Dayna na Davido.

Hata hivyo, Dayna mwenyewe ameliambia gazeti hili kwamba yeye ni mwanamke, hivyo vyovyote anaweza kufanya au kutokea katika maisha yake.

Hata utengenezwaji wa video ya wimbo uliosimamiwa na Kesh Ofuobi, na kisha video yake kuongozwa na Nikmunah, inaaminika imeangamiza pesa nyingi kuliko wanamuziki wengine wa kike.

Hata hivyo, watu wa karibu na Dayna, wanasema wanamuziki hao wawili wamekuwa karibu kiasi ambacho kila siku lazima wawasiliane.

"Hata sisi watu wake wa karibu tuna mashaka kuna zaidi ya kushirikiana kimuziki, kila siku lazima wawasiliane ni jambo zuri, lakini hajaweka wazi kwa sasa," kinasema chanzo hicho.

Dayna mwenyewe amesema kama watu wanafikiria jambo hilo, kwake si tatizo.

"Mimi ni mwanamke nina kila kitu kinachomvutia mwanamume, kama wanafikiria jambo hilo kwangu si tatizo, lakini kwa sasa mashabiki wangu waangalie kazi mpya ili tuendelee kuwa pamoja," amesema Dayna.

Mwimbaji huyo wa vibao kama 'Nivute Kwako', na 'Angejua', tangu alipokuwa nchini Nigeria kuandaa ngoma hiyo, uvumi wa kuwa na uhusiano wa kimapenzi na Davido, ulisambaa kwa kasi katika mitandao ya kijamii.

BASI SAWA

## Muumini awatamani Zuchu, Nandy



MWIMBAJI mkongwe wa muziki wa dansi, Mwinjuma Muumin, amesema, anajiandaa kushirikisha wasanii wa muziki wa kizazi kipya kwenye baadhi ya nyimbo za bendi yake iitwayo Special Band.

Baadhi ya wasanii ambao Muumin amesema atawashirikisha, ni Zuchu, Nandy na wengine ambao anaendelea kufanya nao mazungumzo.

Muumin alisema hayo, kwenye onyesho maalum la utambulisho wa wimbo wa sita wa bendi hiyo utaitwa 'Mkonga wa Tembo'.

"Tumetambulisha wimbo huu wa sita, na kuanzia sasa nitatafuta wasanii wa muziki wa kizazi kipya kuwashirikisha kwenye baadhi ya nyimbo zetu nyingine ili kupata ladha tofauti katika muziki wetu," amesema Muumin.

## Sister P kumbe mgumu tangu zamani



RAPA mkongwe hapa nchini, Sister P, amesema mwonekano wake na kuvaa nguo za kiume, kulimpatia shida kupata wanaume baada ya wengi kuogopa kumsogelea.

Amesema kwake yeye jambo hilo hakuliweka kichwani, kwani suala la kutopenda wanaume lilikuwa nalo tangu zamani.

"Mimi ni mgumu kwa hiyo tangu zamani watu walikuwa wanaogopa kunifuata, walikuwa wananichukulia kama muhuni mwenzao, nahisi walikuwa wanajua wakinifuata naweza nikawapiga hata ngumi". Amsema.



# Chuchu Hans kuandaa Miss Tanga 2021

MSANII wafilamu hapa nchini Chuchu Hans, yupo katika harakati ya kuandaa shindano la Miss Tanga, litakalofanyika mwezi Agosti mwaka huu.

Akizungumza na BT, Chchi Hans amesema kwa sasa anakamilisha mipango ya kuwapata wadhamini ili kulifanya shindano hilo kuwa la kipekee katika ukanda huo.

"Nimepata nafasi ya kuandaa shindano la Miss Tanga, nashukuru kila kitu kinakwenda vizuri na nipo katika hatua ya mwisho kuwapata wadhamini watakaosaidia kulinogesha zaidi," amesema.

Aidha, amewataka wasichana wa mkoa huo wenye sifa kujitokeza kuomba nafasi zinazotakiwa kati ya 15 hadi 20.



# Kiba kufanya kweli

NI mwendo wa bandika bandua! Ndivyo anavyosema staa wa Bogo Fleva, Ali Kiba, akimaanisha katika kipindi hiki cha joto itakuwa ni kukimbiza tu kwa ngoma za moto.

Katika ukurasa wake wa Istagram, Kiba ambaye ni bosi wa lebo ya Kings Music, amewaambia mashabiki wake kuwa baada ya 'Ndombolo' kazi zingine zitaangushwa moja baada ya nyingine.

"Kipindi cha joto kimewadia, tunakwenda kuwafurahisha mashabiki kwa kudondosha moja baada ya nyingine," amesema Kiba.

# 5 zilizoitingisha Twanga

**Na Adam Fungamwango**

WIKI iliyopita bendi ya African Stars 'Twanga Pepeta.' ilizindua albam yao mpya 'Penzi Sigara Kali', kwenye ukumbi wa Break Point Makumbusho jijini Dar es Salaam.

Ilikuwa ni baada ya miaka minane ya kukaa bila kutoa albamu yoyote ile. Mara ya mwisho ilikuwa mwaka 2016 jijini Mwanza ilipozindua albam ya 'Usiyaogope Maisha.'

Twanga Pepeta ni bendi iliyopitia mafanikio makubwa na changamoto nyingi.

Ilianzishwa mwishoni mwa mwanzoni mwa miaka ya 2000.

Baada ya kulitesa soko la muziki nchini, baadaye ziliundwa bendi zenye mlengo kama huo, ambazo zilipa ushindani mkubwa Twanga Pepeta na kunyang'anyana mashabiki.

**TOT PLUS BAND**

Ni bendi ya mwanzo kabisa iliyoanza kuitingisha Twanga Pepeta. Kwanza kabisa ilichofanya ni kumchukua kinara aliyekuwa kwenye kiwango cha hali ya juu na kipenzi cha bendi hiyo, Banza Stone.

Kujiunga kwa Banza kwenye bendi ta TOT kulisababisha upinzani mkubwa wa bendi hizi mbili na pia kuipaisha.

Pili ikawa maarufu na kuwa mshindani halisi wa Twanga Pepeta, kiasi cha kuvuta mashabiki wengi zinapopambana laivu au kupambanishwa kwenye redio na TV.

**MCHINGA SOUND BAND**

Ilianzia mkoani Lindi, lakini ikaja kufanya makazi yake jijini Dar es Salaam. Ni bendi ambayo ilikuja kuisumbua mno Twanga Pepeta, kwa sababu iliwachukua baadhi ya wanamuziki wake kama Adolf Mbinga, Joseph Watugulu, Rogat Hega 'Katapila' na wengineo.

Hali hii ilisababisha mashabiki wa Twanga Pepeta kuiona si bendi rafiki kwao na kukawa na upinzani mkali si kati ya bendi hizo mbili tu, bali hata uongozi wa bendi hizo nao mara kwa mara ulikuwa ukiingia kwenye mzozo.

Chuchu Sound Band

Kama kuna bendi ambayo ilikuja kwa kasi na kuondoka kwa kasi vile vile ni hii. Chuchu Sound ni bendi ndogo tu ambayo iliundwa na baadhi ya wanamuziki wa Kikongo na Kitanzania, lakini ilitesa na kuzoa mashabiki wengi kwa muda mfupi na kuziacha bendi nyingine, ikiwamo Twanga Pepeta zikiulizana.

**FM ACADEMIA**

Baada ya kuipa changamoto Diamond Sound Band, wakati huo ikiitwa FM Musica, ilibadilisha jina na kujiita FM Academia. Sasa ikahamia kuipa wakati mgumu Twanga Pepeta, ikiwa na kina Nyosi El Sadaat. Ni bendi ambayo kwa kipindi kirefu imetoa ushindani mkubwa kwenye muziki wa dansi nchini hasa wa kizazi hicho kuanzia mwishoni mwa miaka ya '90 hadi leo.

**STONO MUSICA 'WAJELAJELA ORIGINAL'**

Historia ya bendi hii haitofautiani na ya Chuchu Sound. Ilikuja kwa moto mkali, lakini ukazimika ghafla. Ilisumbua na kutesa, si kwa Twanga Pepeta tu, bali bendi zote na hasa FM Academia ambapo wanamuziki wengi walitoka huko.

Baadhi ya wanamuziki wa FA Academia raia wa Congo DR walikamatwa kwa kuishi nchini bila vibali.

Walikaa rumande kwa muda na baada ya kutoka walitunga wimbo wa 'Prison' au 'Chozi la Mnyonge,' lakini muda mfupi tu baadaye, walijiengua kwenye bendi yao na kuunda Stono Musica ambayo iliyotoa vibao kama 'Binadamu', 'Jimmy Chocolate,' 'Majivuno' na nyingine nyingi.






# Matusi; Uswahili poa, vijijini tatizo

**Na Adam Fungamwango**

MATUSI ni tamthilia kabambe iliyotungwa na gwiji la utunzi wa filamu, Madebe Lidai. Ni filamu inayoonyesha utofauti wa maisha ya mjini na kijiji. Malezi ya watoto wa mjini na kijijini. Pia tabia ya vijana wanaokulia mjini kwenda vijijini au kinyume chake. Ni tamthilia inayotilia mkazo sana mila na desturi za Kitanzania, hasa zile za unyago kwa vijana wa kiume na kike jinsi ya kujitambua kabla hawajakuwa na familia zao.

Imechezwa na wasanii Madebe mwenyewe, Sorgud Gurdson, Zaudia Shaaban, Haviti Ngokwe, Sabina Athanas, Fidelis Anzigari na Aldis Said.

Bashite kijana kutoka mjini anawasili kwenye kijiji alichozaliwa na kukulia marehemu mama yake. Amekwenda na mpenzi wake Chanuo kwa ajili ya kujitambulisha kwa babu na mjomba wake ili wampe baraka kwani ataka kuoa.

Hata hivyo umjini umewakaa sana. Ile wanafika kijijini walikutana na mzee mmoja, mwanamke akamwambia mpenzi wake kuwa watu wa kijiji hiki wananuka. Mzee alikasirika, akajiapiza kulipa kisasi.

Tabia za msichana huyo ziliwachefua babu na mjomba wa Bashite. Nguo za kimjini, kuongeza na heshima yake, haikuendana na utamaduni wa kijiji kile.

Lidai ambaye ni mjomba wa Bashite alijitahidi sana kumwambia mpwaye na msichana.

Anawaambia kama anataka kutoa baraka, basi ni lazima msichana huyo achezwe kwanza unyago kwa sababu anavyoonekana hana tabia nzuri.

Msichana aliona kama anateswa au kunyanyaswa. Akaamua kutoroka. Hata hivyo njiani aliangukia kwenye penzi la kijana mwingine kijijini hapo anaitwa Batani. Pia ana mke. Kumbe Batani alitumwa na mzee aliyetukanwa na msichana yule kuwa ananuka siku alipoingia kijijini. Batani ni mmoja wa vijana wa mzee huyo aliyewafanyia tohara. Kumbe mzee yule ni ngariba.

Habari zinatapakaa kijijini hapo. hali ya hewa inachafuka. Lakini Madebe anajitahidi kutuliza hali hiyo.

Ngariba akasema ni yeye ndiye aliyemtuma kijana wake huyo Batani kwa sababu ya kumfundisha adabu msichana huyo, kwani alimtukana wakati anaingia kijijini hapo kwa kumwita mchafu na ananuka.

Bashite hamtaki tena mchumba wake kwa sababu katembea na kijana wa kijijini. Madebe anatuliza hali ya hewa.

Hatimaye kila mmoja akajiona ni mkosaji kwa wakati wake. Chanuo akasema kuna vitu amejifunza kutokana na tukio hilo, na akaomba msamaha, huku akianza sasa kwenda hata kuchoma maji kisimani.

# Meghan, prince Harry matatani kumuita mtoto jina la malkia




UTATA umeibuka kuhusu jina la mtoto wa pili wa Prince Harry, baada ya kudaiwa jina alilopewa la Lilibet, hakupata ruhusa kutoka kwa bibi yake ambaye ni Malkia Elizabeth wa uingreza.

Ripoti moja inadai kuwa jina hilo ambalo ni la utani la Malkia Elizabeth, Harry na Meghan walimpatia mtoto wao bila kupata baraka kutoka kwa kiongozi huyo.


Chanzo kutoka kasri la kifalme, zinasema Malkia hakuulizwa na Meghan wala Harry, juu ya utumiaji wa jina lake la utani.

Hata hivyo, Harry amesema aliomba ruhusa kutoka kwa Malkia kumwita mtoto wake mchanga "Lilibet", lakini wasemaji wa kifalme wanasema Malkia hakuwahi kuulizwa.

Msemaji rasmi wa Prince Harry na Meghan Markle ambaye ni mwigizaji wa Hollywood, amesema mwanamfalme huyo alizungumza na familia yake mapema kabla ya tangazo.



## West aopoa mtoto mwingine



RAPA maarufu wa Marekani, Kanye West, inadaiwa yupo katika mapenzi mazito na mwanamitindo wa kimataifa kutoka Ufaransa, Irina Shayk.

Taarifa kutoka vyanzo mbalimbali, vinaeleza wawili hao walikutwa pamoja wakati msanii huyo alipokuwa nchini humo kwa ajili ya sherehe ya kutimiza miaka 44 ya kuzaliwa kwake.

Picha zilizotolewa na gazeti la Daily Mail, walionekana wakifurahia maisha katika mitaa mbalimbali siku ya Jumanne ya wiki hii.

Kanye West na mkewe, Kim kardashian, wapo katika harakati za kisheria za kupeana talaka baada ya kuwapo sitofahamu kwa muda mrefu kati yao.

## Binti wa Waje ana vituko!

MSANII mkongwe wa filamu kutoka Nigeria, Waje, amefunguka kwamba binti yake huwa anamchunguza pale anaporudi nyumbani akiwa amelewa.

Staa huyo amesema hayo wakati anazungumza na Ebuka Obi-Uchendu, kwenye kipindi cha Rubbin Minds.

Kulingana na Waje, uzazi hauna mwongozo kamili na inafikia wakati watoto wanajifunza mengi kupitia wazazi, hasa wale wasio na wenza.





## Akon kweli wewe kidume

MWANAMUZIKI wa Marekani mwenye asili ya Senegal, Akon, amewaacha watu na butwaa baada ya kusema hana mpango wa kumshtaki mtu aliyeiba gari lake la kifahari.

Gari hilo aina ya Range Rover, liliibwa wakati akiwa kituoni akiongeza mafuta, lakini alifanikiwa kulipata baada ya kushirikiana kwa ukaribu na polisi.

Chanzo cha karibu na mkongwe huyo kimeeleza kwamba hana mpango wa kuwasilisha malalamiko mahakamani, bali anafikiria namna gani anaweza kuondoka mtaani hapo ili kuachana na tabia hizo.

## JLo, Ben wazidi kujirusha

MWIGIZAJI nyota wa Marekani, Ben Affleck na aliyekuwa mke wake Jennifer Lopez, wamezidi kuwapa presha watu baada ya penzi lao kurudi likiwa moto.

Ben na Jlo, ambao waliachana mwaka uliopita, walianza kuonekana pamoja Mei 31, mwaka huu wakiwa katika mahaba mazito.

Wawili hao wamechukua vyumba katika hoteli ya kifahari ya Pendry iliyoko West Hollywood, Calfonia wakila maisha kwa furaha.



MAKALA

# FURAHA YA MIUJIZA

## ●Simulizi ya aliyejifungua watoto 10
## ●Madaktari washindwa kuona wawili

**Na mwandishi Wetu**

TUKIO la miujiza, lakini kwa Gosiame Thamara Sithole, kwake limetokea kweli na kuamini kuwa Mungu akipanga, basi kila kitu kitakwenda kama kinavyotakiwa.

Mwanamke huyo wa Afrika Kusini, sasa ameingia katika rekodi mpya ya Dunia baada ya kujifungua watoto 10 kwa pamoja.

Idadi hiyo ya watoto iliwashangaza watu wengi, kiasi ambacho baadhi waliita tukio hilo kama miujiza yaliyofanywa na Mungu ili kuonyesha uwepo wake.

Mume wake Gosiame anasema, hata wao wenyewe walishangazwa na idadi hiyo ya watoto, kwani katika picha ya scan ilionyesha mke wake alikuwa na watoto wanane tu tumboni mwake.

Hata hivyo, kuzaliwa kwa watoto hao kumeleta furaha nchini humo, kiasi ambacho serikali imewapongeza wazazi na kuwatakia afya njema watoto hao.

"Ni wavulana saba na wasichana watatu. Nina furaha. Ninahisia. Siwezi kuzungumza mengi," Teboho Tsotetsi ambaye ni baba wa watoto hao aliiambia gazeti la Pretoria News.

Ofisa mmoja wa Afrika Kusini, aliithibitishia shirika la utangazaji la Uingereza (BBC) kuhusu kuzaliwa kwa watoto hao.



Gosiame Thamara Sithole

Mmoja wa watu wa familia yao, ambaye hakutaka kutambuliwa, aliiambia BBC kuwa Bi Sithole alipata watoto 10, kati ya hao watano alijifungua kwa njia ya kawaida na watano wengine kwa njia ya upasuaji.

Kutokana na tukio hilo, taasisi ya rekodi ya dunia ya Guinness, ilisema inachunguza kisa hicho.

Mpaka sasa mwanamke wa Marekani ambaye alijifungua watoto wanane, ndiye anayeshikilia rekodi ya Guiness ya mtu aliyejifungua watoto wengi zaidi mara moja anayeishi.

Katika tukio kama hilo lililoripotiwa mwezi uliopita, mwanamke mwenye umri wa miaka 25, Halima Cisse kutoka nchini Mali, alijifungua watoto tisa.

Halima alijifungua watoto hao katika hospitali moja nchini Morocco, na afya zao zinaendelea vizuri.

Mara nyingi mimba nyingi zenye idadi kubwa ya watoto huishia kuharibika.

Hata hivyo, uzazi wa watoto zaidi ya watatu inakuwa nadra kutokea na mara nyingi hutokana na utungaji mimba wa kitaalam.

Lakini wanandoa hao wanasema wao ni tofauti kwani ujauzito ulitungwa katika njia ya kawaida .

**HALI NGUMU**

Gosiame ambaye ana umri wa miaka 37, awali alijifungua watoto mapacha ambao kwa sasa wana umri wa miaka sita.

Alisemekana alikuwa mzima mwenye afya baada ya kujifungua baada ya kutimiza wiki 29 katika hospitali mmoja mjini Pretoria.

Hata hivyo, anasema ujauzito wake ulikuwa na hali ngumu ngumu mwanzoni, kiasi ambacho ilimfanya kumuomba Mungu angalau kumuondolea baadhi ya kero.

Ilikuwa vigumu kwake kukaa kama watu wengine na usiku alishindwa kupata usingizi kutokana kuwa na mawazo mengi kuhusu kitakachomtokea wakati wa kujifungua.

"Niliwaza vipi watatosha tumboni mwangu? Wataweza kuishi vipi?" nilijiuliza mwenyewe.

Swali hilo alikuwa akiwauliza hata madaktari wake, lakini walimtuliza kwa kumwambia mji wa mimba ulikuwa ukitanuka na hivyo itakuwa rahisi watoto hao kuishi.

Katika kipindi chote cha mawazo na maswali mengi, bado alikuwa akifahamu alibeba mimba ya watoto wanane pekee.

Katika hali hiyo ya mashaka uchunguzi uliofanywa na madaktari walibaini Bi Sithole alikuwa anaumwa miguu kutokana na watoto wawili kati ya wanane walikuwa katika mrija usio sahihi.

"Hilo lilitatuliwa na nimekuwa sawa tangu wakati huo. Natamani kuwaona watoto wangu," alieleza.

Mume wake pia anasema alikuwa mwenye furaha ya kupindukia, na alihisi kama mmoja wa watoto waliochaguliwa na Mungu.

" Ni muujiza ambao ninaushukuru ". aliongeza kusema.



Watoto wakiwa katika vyombo maalum vya kuwatunza



Gosiame akiwa na mume wake, Teboho Tsotetsi

# NEC: Huu uchaguzi mdogo ndio mlango wa demokrasia

## ■Yaandaa 'kipenga' majimbo, kata zinazosubiri

**Na Bartholomew Wandi**




Shughuli za upigaji kura zikiendelea. **PICHA: MTANDAO.**

UCHAGUZI wowote ule uwe mkubwa au mdogo, ni muhimu kwa kukuza demokrasia na kutoa fursa kwa wananchi, kuchagua kiongozi wao wanayemtaka au kuchaguliwa.

Tofauti ya Uchaguzi Mkuu na Uchaguzi Mdogo ni kwamba Uchaguzi Mkuu unahusisha kumchagua Rais na wabunge nchini, pia wawakilishi na masheha kwa upande wa Zanzibar.

Ni uchaguzi unaofanyika kila miaka mitano, baada ya Rais kulivunja rasmi Bunge kwa mujibu wa sheria.

Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), huratibu na kusimamia uchaguzi mkuu wa Rais na wabunge wa Tanzania na madiwani wa Tanzania Bara, pia Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC) inasimamia uchaguzi wa Rais wa Tanzania Zanzibar, wawakilishi na masheha.

Uchaguzi mdogo upo kwa ajili ya wabunge na madiwani Tanzania na Zanzibar, zikihusisha wawakilishi na masheha.

Kisheria, hakuna uchaguzi mdogo wa Rais. Inapotokea, kiti cha Rais kuwa wazi kutokana na kifo, kujiuzulu, kupoteza sifa za uchaguzi au kutomudu kazi zake kutokana na maradhi, Makamu wa Rais ataapishwa kuchukua nafasi, kama ilivyotokea nchini hivi karibuni.

Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inafafanua uchaguzi mdogo wa ubunge na udiwani unafanyika baada ya uchaguzi mkuu wa rais, wabunge na madiwani.

Hiyo inatoa mantiki, Tanzania ina chaguzi ndogo za ubunge na udiwani, pia Wawakilishi na Masheha Zanzibar. Hata hivyo, mara nyingi hawathamini chaguzi ndogo kama ilivyo uchaguzi mkuu, kiasi kwenye kampeni na siku ya kupiga kura hujitokeza watu wachache sana.

Kimsingi, ni tendo linalowakosesha haki ya kikatiba ya kupata habari muhimu kutoka kwa wagombea wanaoelezea sera zao, pia wasikilizaji wanatafakari, hatimaye wanatumia haki yao kidemokrasia kumchagua kiongozi anayewafaa kwa maendeleo.

Ni hali inayotoana na ushabiki kichama na kulalamikia kiongozi hafai, baada ya kuchaguliwa hatua inayofaa kufanyiwa kazi kupitia wa fursa za mapema.

**NAMNA INAVYOELEKEA**

Spika wa Bunge huitaarifu kisheria Tume Taifa ya Taifa ya Uchaguzi. Siku za uteuzi si chini ya siku 20 na haizidi 50, baada ya kutokea tukio linalosababisha uchaguzi.

Uchaguzi mdogo wa udiwani hufanyika kwa Waziri mwenye dhamana wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), anayetangaza kuwapo kiti wazi cha diwani, baada ya kupewa taarifa ya maandishi na mwenyekiti wa halmashauri husika.

Sababu za uchaguzi mdogo wa ubunge na udiwani kufanyika ni iwapo mbunge au diwani, ama amefariki au kajiuzulu; au kupitia sababu nyingine ni anatangazwa batili; kiti cha ubunge na udiwani unachukuliwa wazi au anakoma kuwa mwanachama wa chama kilichomdhamini ubunge au udiwani wake; mkasa wa kutenguliwa na mahakama.

Sheria inainisha kwamba uchaguzi mdogo wa Ubunge na Mjumbe wa Udiwani, hautafanyika ikiwa imebakia miezi 12 kufanyika Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani.

**UCHAGUZI MDOGO**

Zanzibar mnamo Julai 18, 2021 kutakuwapo Uchaguzi Mdogo wa Ubunge katika jimbo moja la Konde, katika Halmashauri ya Wilaya Micheweni, kisiwani Pemba.

Pia, kuna uchaguzi wa Udiwani katika kata sita za Mbagala Kuu katika Halmashauri ya Manispaa ya Temeke, mkoani Dar es Salaam; Ndirigish katika Halmashauri ya Wilaya Kiteto, Manyara; na Mitesa katika Halmashauri ya Wilaya ya Masasi.

Mengine ni Halmashauri ya Wilaya Newala, mkoani Mtwara, Gare katika Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto, Mkoani Tanga na Chona katika Halmashauri ya Wilaya Ushetu, mkoani Shinyanga, baada ya Wawakilishi hao kufariki dunia.

Uchaguzi huu Mdogo wa Ubunge na Udiwani ni wa pili tangu kumalizika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020.

Majimbo na kata ambayo tayari yameshafanya Uchaguzi Mdogo ni katika Majimbo mawili ya Muhambwe wilayani Kibondo na Buhigwe Buhigwe Mkoani Kigoma, yote mkoani Kigoma.

Pia, kwa udiwani kuna kata tano za Buziku, iliyoko Chato; Bugalama wilayani Geita; Igunga mkoani Tabora; Miuta, Mtwara; na Ligoma Tunduru.

Aidha, kabla ya uteuzi kuna kata wazi 16, lakini baada ya uteuzi wagombea kutoka kata 11 walipita bila kupingwa, kata na halmashauri zao ziko katika mabano: Jana (Msalala), Kising'a (Kilolo), Igusule (Nzega), Sagara (Kongwa), Matembwe (Njombe), Engutoto (Monduli), Kisiwani (Bumbuli), Iwiji (Mbeya), Mhezi (Same), Kikongo (Kibaha) na Mmale (Uyui)

Hadi sasa NEC imepanga uchukuaji fomu za Uteuzi wa majina kwa wagombea wa uchaguzi mdogo wa ubunge katika Jimbo la Kondena na uchaguzi mdogo wa udiwani wa kata hizo sita, utafanyika kati ya tarehe 21 na 27 mwezi huu.

**UTEUZI, KAMPENI, KURA**

Kampeni za uchaguzi huo mdogo kwa ajili ya ubunge na udiwani zitaanza tarehe 28 mwezi huu na kudumu kwa wiki tatu zikiishia Julai 17, siku moja kabla ya tarehe ya uchaguzi, Julai 18 mweaka huu.

Angalizo la Tume ya Uchaguzi ni wagombea wote watakaoteuliwa kwa nafasi za ubunge na udiwani wayaheshimu, kuyazingatia na kuyafuata maadili ya uchaguzi, yaliyotolewa kwa Uchaguzi Mkuu wa Rais, wabunge na madiwani ya Mwaka jana.

Tume ya Uchaguzi inasema, Daftari la Kudumu la Wapiga Kura litawekwa wazi katika vituo vyote vya kupigia kura katika jimbo hilo moja na kata sita, zikiwa wazi vituoni kwa nane, kabla ya uchaguzi yaani kati ya Julai 10 na 17 mwaka huu.

Dhumuni kuu ni kuhakiki majina mapema na vituo vya kupigia kura vitafunguliwa kati ya saa 1:00 asubuhi na kufungwa saa 10:00 Jioni, wapiga kura wanatakiwa kwenda katika vituo vya kupigia Kura wakiwa na kadi za kupigia kura.

Wakati atakayeruhusiwa ni raia wa Tanzania aliyeandikishwa katika Daftari la Kudumu, sharti lingine ni kwa mmpiga kura awe na kadi halisi ya kupigia kura, ikiwa ni maelekezo ya Sheria ya Uchaguzi.

Kwenye Uchaguzi huo wa Ubunge katika majimbo mawili na Udiwani kwenye kata tano Tume ya Taifa ya Uchaguzi imeelekeza wapiga Kura walioandikishwa katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura mwaka 2015 na 2019/2020 na wamepoteza kadi, kufutika picha na maandishi au kukatika, watapiga kura kwa kutumia hati za kusafiria, Kitambulisho cha Taifa au leseni ya udereva, ambazo picha na majina yanafanana na kwenye daftari.

Pia, angalizo, ni muda uliotangazwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi na utakapoisha, hakuna mtu atakayeruhusiwa kupiga kura, ila tu wale utakaowakuta wapo kwenye mstari.

■ **Mwandishi wa Ofisi Habari Mkuu wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), Simu: + 255 754 203015**

# Ajira utotoni tishio zafikia milioni 160

**Geneva,** USWISI

KWA mara ya kwanza katika kipindi cha miongo miwili, ajira za ututoni zimeongezeka na kufikia watoto milioni 160.

Huenda takwimu hizo zikapanda kwa mwaka ujao wa 2022 iwapo hatua za haraka hazitachukuliwa kuwalinda watoto.

Taarifa hiyo ni kwa mujibu wa ripoti iliyotolewa jana na Mashirika mawili ya Umoja wa Mataifa lile la kushughulikia watoto UNICEF na la ajira ILO mjini Geneva Uswisi.

Ripoti hiyo ya ILO na UNICEF ambayo imetolewa kuelekea siku ya kupinga ajira za ututoni Juni 12, imeeleza namna familia zilivyofanya uamuzi mgumu kwa watoto wao kuingia kwenye ajira ilihali wana umri mdogo na kinachohuzunisha zaidi ni kuwa, watoto kati ya miaka mitano mpaka 11 ndio wengi zaidi ukilinganisha na watoto wenye umri kati ya miaka 11 mpaka 17.

Pia imeonya watoto milioni tisa, wapo kwenye hatari ya kuingia kwenye ajira ifikapo mwaka 2022, kutokana na athari za janga la corona na iwapo hatua za haraka hazitachukuliwa idadi hiyo inaweza kuongezeka na kufikia milioni 46.

"Tunapoteza muelekeo katika vita hii ya kukomesha ajira za ututoni" alisema Mkurugenzi Mtendaji wa UNICEF Henrietta Fore

"Sasa ukiwa ni mwaka wa pili kujifungia ndani kupambana na corona, shule kufungwa uchumi kuathirika na kushuka kwa bajeti za kitaifa, familia zimefanya uamuzi mgumu.

"Tunazishauri serikali na benki za maendeleo kuwekeza katika programu zitakazowatoa watoto kwenye ajira na kuwarejesha shuleni, pia kuzisadia familia, ili kuacha kufanya uamuzi mgumu wa kuruhusu watoto wadogo waingie kwenye ajira."

Ripoti ilibainisha katika ukanda wa jangwa la Sahara, ndani ya miaka minne watoto milioni 16.6 wameingia kwenye ajira na wengi wao kutoka vijijini.

Mkurugenzi Mkuu ILO, Guy Ruder alisema ni dhahiri wameshindwa kuwalinda watoto.

"Takwimu hizi zinatuamsha kutoka kwenye usingizi, hatuwezi kuacha kufanya kitu wakati kizazi kipya kipo hatarini. Tukifanya ulinzi wa pamoja tutasaidia familia kuhakikisha watoto wao wanabaki shuleni hata wanapopatwa na hali mbayá ya kiuchumi.

"Kuongeza uwekezaji vijijini na kwenye masuala ya kilimo, huu ni wakati wa kuhakikisha tunavunja mzunguko wa umasikini na ajira za ututoni,"alisema mkurugenzi huyo.

Asilimia 70 ya watoto wameajiriwa kwenye sekta ya kilimo, ikifuatiwa na huduma ambayo ni asilimia 20, na asilimia 10 iliyobaki ni kwenye viwanda.

**UN**




Rais wa Marekani, Joe Biden and Waziri Mkuu wa Uingereza, Boris Johnson, wakizungumza kabla ya kushiriki mkutano wa mataifa yenye nguvu kiuchumi duniani, G-7 mjini, Carbis Bay, Uingereza. **PICHA: AP**

# Ufaransa mikakati vita dhidi ya ugaidi kubadilika

**Paris,** UFARANSA

RAIS Emmanuel Macron, ametoa wito kutaka kubadilishwa kwa kina uwepo wa jeshi la Ufaransa katika ukanda wa Sahel,

Macron aliyasema hayo katika mkutano na waandishi wa habari juzi jioni.

"Kwa kweli, hii inamaanisha kupunguzwa kwa wanajeshi wa Ufaransa katika eneo hilo na mwisho wa Operesheni Barkhane kama operesheni ya nje ya nchi, kwa faida ya muungano wa kimataifa unaoleta pamoja mataifa ya ukanda huo na Ulaya.

"Mfumo huu wa kuwepo kwetu huko Sahel hauendani tena na hali halisi ya mapigano," alisema Rais Macron.

Alisema tangazo lililotolewa juzi kwamba Ufaransa inajiondoa katika ukanda wa Sahel haimaanishi itapunguza vikosi vyake.

Macron alizungumzia wanajeshi wa Ufaransa watapunguzwa kutoka zaidi ya 5,000 hadi mia kadhaa.

Alitaja pia kufungwa kwa baadhi ya vituo vya jeshi la Ufaransa, bila kubainisha vituo hivyo, akisema lengo ni kutoa ulinzi katika maeneo makubwa ambapo nchi husika zinajaribu kudhibiti hali ya mambo.

"Ushirikiano uliowekwa karibu na kikosi cha Ulaya Takouba, kilichozinduliwa mwezi Machi 2020, na kimetolewa wito wa kuimarisha vikosi vyake" alisema Macron.

"Ufaransa itabaki kuwa uti wa mgongo wa kikosi hiki ambacho majeshi mengine ya Afrika na ya kimataifa yatashirikishwa.

**RFI**

# Mkutano G7 waegemea janga corona

**Cornwall,** UINGEREZA

MKUTANO wa kilele wa kundi la mataifa tajiri na yaliyoendelea zaidi kiviwanda la G7, umeanza katika mji wa mwambao wa Cornwall nchini Uingereza, huku janga la virusi vya corona likigubika mazungumzo hayo ya siku tatu.

Sehemu ya viongozi wa wakuu wa mataifa ya kundi hilo wanaendelea kuwasili kwenye hoteli ya fahari ya Carbis Bay, iliyo kwenye fukwe za mji wa Cornwall kwa mkutano huo wa G7 utakaojaribu kutafuta majibu kuhusu janga la virusi vya corona na hatua nzito nzito za kuufufua tena uchumi wa dunia.

Rais wa Marekani, Joe Biden na mwenyeji wake Waziri Mkuu wa Uingereza, Boris Johnson, walikuwepo mjini humo tangu Jumatano na jana walikuwa na mazungumzo mapana kuhusu ushirikiano kati ya Washington na London.

Viongozi wa mataifa mengine ya kundi hilo, linalojumuisha pia Ujerumani, Japan, Canada, Italia na Ufaransa walitarajiwa kuwasili Cornwall KUSHIRIKI mkutano huo ambao ni kwanza kufanyika ana kwa ana tangu kuzuka janga la corona karibu miaka miwili iliyopita.

Suala la chanjo za Covid-19 ni kitovu cha majadiliano

Baada ya mkutano dhifa ya chakula cha pamoja iliyoandaliwa na Malkia Elizabeth wa Pili, ilifanyika.

Duru zinasema viongozi wa G7 watajadili kwa kirefu suala la chanjo za CoVID-19 wakilenga kutoa ahadi ya msaada wa dozi bilioni moja za chanjo kwa mataifa masikini na msaada wa kifedha wa kujenga vituo zaidi vya kuzalisha chanjo duniani.

Viongozi wa kundi hilo wanaandamwa na shinikizo la kuwataka kutangaza mipango ya kutoa msaada wa chanjo, kufuatia malalamiko kwamba hakuna usawa katika usambazaji wa chanjo duniani

Kuelekea mkutano huo, Rais Biden alisema Marekani itachangia dozi milioni 500 nyingine kwa mataifa 92 masikini na kwa Umoja wa Afrika (AU) kabla ya Juni mwaka ujao.

"Tutaendelea kuzalisha chanjo, kutoa msaada wa dozi, kutoa ajira, kama wanavyosema hapa Uingereza, silaha mkononi, hadi dunia ivishinde virusi hivi" alisema Biden.

**DW**

# Algeria kufanya uchaguzi leo

Algiers, ALGERIA

ALGERIA inafanya uchaguzi wa bunge leo, wakati vuguvugu la maandamano likisihi wapigakura kususia, huku kukiwa na wasiwasi kwamba taifa hilo la Afrika Kaskazini linaweza kujikwamua kutoka kwenye janga la kisiasa na kiuchumi.

Serikali ya nchi hiyo inajaribu kuimarisha uhalali wake, huku ikikabiliana na vuguvugu la Hirak, ambalo limerejea tena barabarani Februari, baada ya kusitisha maandamano kwa karibu mwaka mmoja kufuatia janga la corona.

Mwaka wa 2019, Hirak liliongoza maandamano ya maelfu ya watu na kupelekea kujizulu kwa kiongozi wa muda mrefu wa taifa hilo, Abdelaziz Bouteflika baada ya kutangaza nia ya kuwania urais kwa muhula wa tano.

Uchaguzi wa urais uliyofanyika miezi 18 iliyopita, ulishindwa na Abdelmadjid Tebboune, wakati ukiwa na chini ya asilimia 40 ya wapiga kura walioshiriki kulingana na takwimu rasmi.

Alhamis kiongozi wa upinzani Karim Tabbou, alikamatwa karibu na nyumba yake kulingana na ripoti iliyotolewa na ndugu yake.

**VOA**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**IBRAHIM SAPI MKWAWA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S342/147** kilichotolewa na Baraza la Mitihani kupitia SHAABAN ROBERT SEKONDARI mwaka 1984. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **DAR/CEN/RB/295765/2021.**

## KUPOTEA KWA VYETI



**MIMA ATHUMANI ALIASA** anatangaza kupotelewa na cheti che kidato cha nne chenye index namba ***S4777-0017*** kilichotolewa na NDURUMO SEKONDARI mwaka 2013. Cheti cha Chuo chenye namba **ACE/0015** kilichotolewa na ALHARAMAIN COLLEGE OF EDUCATION mwaka 2017. Transcript yenye namba **ACE/0015.** Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/CHA/RB/235294/2021.**

## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI

**MGEN TANZANIA INSURANCE COMPANY LTD** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA BAJAJI YENYE NAMBA ZA USAJILI **MC 706 AUV.** CHASSIS NAMBA **MD2A25B24FWC60072.** ENGINE NAMBA **AZZWFC62104.** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: **DAR/URA/RB/296137/2021.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**WUZHOU INVESTMENT COMPANY LTD** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI AINA YA **SANLG** YENYE NAMBA ZA USAJILI **MC 986 BXG.** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: **KHM/RB/302/2021.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**SKOL BUILDING CONTRACTORS LTD** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 393 BCG** - NISSAN ATLAS. CHASSIS NAMBA **JH40014387.** ENGINE NAMBA **BD30009189.** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: **DAR/URA/RB/296006/2021.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**MWARAMI SWALEHE MAPENZI** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S.2576/0021** kilichotolewa na Baraza la Mitihani kupitia KIBATA SEKONDARI mwaka 2014. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **DAR/URA/RB/293814/2021.**

***Uza,***

***Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi***

***Kwa Bei Poa***

***Tupigie 0782253676***

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HADITHI

# HADITHI

MWANZONI ilionekana ni fahari. Wazazi kupata mtoto wa kike. Akaja kuwa msichana mzuri aliyeumbwa akaumbika na kutamaniwa na kila mtu, ni sifa kubwa. Wakati mwingine mzazi hupata hata vizawadi vidogo kutoka kwa watu mbalimbali bila kujua kuwa nia ni kutengeneza mazingira kwa binti yao. Kinyume chake mzee Ngoma na mkewe Fatuma wanapata mtoto wa kike Bishada ambaye anaondokea kuwa tishio kwenye kijiji cha Mtakuja kwa urembo wake.

Badala ya kuwa tija na faraha kwa wazazi wake anageuka kuwa balaa. Wazazi wanakuwa hawana amani kutokana na vitisho mbalimbali ikiwemo kuuawa kutoka kwa watu mbalimbali ndani na nje ya kijiji hicho. Inakuwa tafrani. Kijiji hakikaliki. watu wanatafutana. Moto unawaka. Bishada mwenyewe maisha yake yanakuwa hatarini. Fuatilia kisa hiki ambacho kitakuacha mdomo wazi.

# Aolewe au afe-**10**

**Mtunzi anapatikana (0716 350534)**

**Na Adam Fungamwango**

"Hapana hapana, msimuua binti yangu. Niueni mimi basi, huku muacheni hana kosa lolote..." Mzee ngoma alipaza sauti yenye hofu.

"Mzee hii tenda tu tumepewa sisi na watu ambao binti yako amewakataa, kwa hiyo hatuwezi kufanya kinyume na hapo."

Haraka Denny alijitosa kwenye kichaka ili kuangalia zaidi tukio hilo bila kuonekana.

Alichoona ni vijana wanne, mmoja akiwa ameshika panga, wawili fimbo na mmoja kisu.

Denny tayari alishaambiwa kila kitu kuhusu familia ile. Ni familia ambayo haipendwi kijijini hapo kutokana na msichana mrembo Bishada kukataa kuolewa na mtu yoyote hapo, hivyo amezua chuki.

Kwa maana hivyo alijua hakukuwa na msaada wowote utakaotolewa. Pia vijana wale kwa walivyojieleza ni kwamba wametumwa.

Alivuta taswira kama asingerudi sijui ingekuwaje. Alinyata na kusogea karibu. Alikuwa ameshawazungukia kwa nyuma. Sehemu ambayo wao wanaangalia mbele, yeye alikuwa nyuma yao.


Alijipapasa mfukoni, bastola yake ilikuwepo. "Ngoja niwafanyie mchezo mmoja ambao utakuwa mfano kwa kijiji kizima." Alijisemea.

Alichomoa bastola yake na kutoka kwenye kichaka haraka akielekea kwenye tukio.

"Nyie wapuuzi wekeni chini silaha zenu, vinginevyo nitamtoa mtu utumbo, pumbavu nyinyi." Aliunguruma.

Uliofuatia hapo ni mshtuko. Kwa wahalifu ulikuwa ni mshtuko maradufu kwa sababu hawakutegemea kukutana na hali ile. Walichokijua wao ni kwamba mgeni yule alikuwa ameshaondoka. Hivyo walivamia pale kumuua Bishada. Baada ya hapo waende kuvamia nyumbani kwa mzee Malilo, wakammalize mgeni huyo. Ilionekana ujio wa mgeni ni hatari kwa wanaume wote kijijini hapo, kwani baada ya kumuokoa Bishada kwa sasa ameonekana kuwa naye karibu zaidi.

Nyendo zao zote zilikuwa zinafuatiliwa. Kama vile haitoshi, Denny aliachia risasi moja juu iliyotoa mshindo mkubwa na kutetemesha kijiji. Kila mmoja alipatwa na hofu. Hawakujua ni kitu gani kimetokea.




*******************************

"Mwenyekiti hiki kijiji chako kina matatizo makubwa. Siku chache tu nilizokaa hapa,a nimegundua kuwa wewe ambaye umepewa jukumu la kulinda wanaanchi wote bila kubagua, ni kama umeitenga familia ya mzee Ngoma."

"Kijana una ushahidi na unachokisema?"

"Ushahidi wa kimazingira unaonyesha hivyo mzee Mataulo."

"Kama upi?"

"Jambo lolote linalotokea kwa mzee Ngoma hulipi uzito, halafu unaonekana kama unawakandamiza."

"Sikiliza, wewe bado kijana mdogo. Mimi nilikuwa rafiki sana wa mjomba wako mzee Malilo, lakini wewe mpwa wake unataka kuleta habari zako za mjini. Hapa wanakijiji wote ni sawa."

"Hapana Mwenyekiti. Siku nilipokuja tu, Bishada alitaka kubakwa. Mtuhumiwa nilimleta hapa. Juzi kavamiwa kule, kukosa mimi matukio haya yote si familia hii ingekuwa imeteketea? Halafu umeniita hapa, badala ya kunipongeza, unaniambia eti mimi nimeanza kukifanya kijiji kukosa na amani. Amani ipi wakati mimi natetea baadhi ya wanakijiji wanaonyanyaswa na kukosa msaada?"

Yalikuwa ni maneno makali ya Denny mbele ya Mwenyekiti Mataulo. Alishindwa kujibu.

Ni kweli mzee Mataulo alikuwa mmoja wa wanakijiji wengi ambao waliingia kwenye kumbo wa kutoipenda familia ya mzee Ngoma. Sababu ni ile ile. Bishada. Hata yeye mwenyewe kwa kutumia cheo chake cha uongozi alishawahi kumtongoza Bishada na kumhakikisha usalama wake kama atamkubali.

Bishada alikataa kama kawaida yake. Kwa hiyo naye aliingia kwenye mtego uleule.

Denny alionekana ni hatari kwenye mpango wa kutaka kumtimua mzee Ngoma na familia yake kwenye kijiji kile.

Pamoja na kuonekana kuwa ana uwezo wa kupigana na silaha ya bastola, lakini alionekana ana elimu ya uraia kwa sababu ya kuishi mjini.

"Kijana fuata kilichokuleta uondoke. Mambo ya huku wewe huyawezi." Mwenyekiti Mataulo alijikuta akijibu.

"Haya hebu nieleze mimi nina kosa gani?" Denny aliuliza. Alikuwa ameitwa kwenye Ofisi ya Kijiji baada ya mlio wa bastola kusikika kijijini hapo, kitu ambacho kilipingwa na baadhi ya wanakijiji kuwa kimesababisha hofu, wasiwasi, na amani kuvurugika.

Na ilipobainika kuwa ilikuwa nyumbani kwa mzee Ngoma, ndiyo kabisa.

Wanakijiji hao hao, wengi wao ndiyo waliounda kikundi cha kwenda kumdhuru mzee huyo, familia yake, ikiwezekana na yeye mwenyewe Denny.

**Uliofuatia hapo ni mshtuko. Kwa wahalifu ulikuwa ni mshtuko maradufu kwa sababu hawakutegemea kukutana na hali ile. Walichokijua wao ni kwamba mgeni yule alikuwa ameshaondoka.**

"Nimekwita kukuonya. Mimi sitaki kufanya kitu chochote. Usirudia tena kupiga risasi. Umeshtua watu wengi. Kijiji chote kina hofu. kwa hiyo nakuonya."

"Ina maana mimi nimefanya kosa kupiga risasi juu? Nimefanya hivyo kwa sababu ya kuwaokoa wanakijiji wako. Na hata wale wavamizi baada ya kufanya hivyo wamekimbia. Lakini sawa nimekuelewa." Mazungumzo wa Denny na Mwenyekiti wa Kijiji, Matulo yakaishi hapo.

************************

"Baba kasema kuanzia leo ukalale nyumbani hadi siku ambayo tunaondoka."

Ilikuwa ni sauti ya Bishada ikimwambia Denny, muda mfupi tu baada ya kutoka kwenye Ofisi ya Kijiji.

Baada ya kuona muda unapita, Bishada alitumwa kwenda kumuangalia mgeni na kama kuna lolote basi akawaambie.

Familia ya mzee Ngoma tayari ilishamuona Denny kama mkombozi wao, hivyo pamoja na wao kuonekana kulindwa, lakini pia na wao hwakutaka wampoteze au baya lolote limpate.

Alionekana ni kama masiya aliyekuja kuwakomboa, au kutatua matatizo yote yaliyokumbana nayo tangu nyuma. Kwa bahati nzuri walikutana njiani.

"Siyo kwangu tena?"

"Baba hatoweza kukwambia. Lakini amemwambia mama na mama kaniambia mimi. Baada ya kunusurika jana, baba amesema wewe ukae nyumbani hadi siku zetu tano zilizobaki za kuishi kijiji hapa."

"Sasa Bishada, hivi tayari mnapo kwa kwenda?"

"Sijui baba. Atakuwa amepata kijiji cha kuhamia."

"Kwa nini usikubali tu barua ili muendelee kuishi hapa? Unajua wewe ndiyo unayemfadhaisha mzee wako?" Denny alimwambia Bishada huku akiwa amemshika mkono wakielekea nyumbani.

"Sitaki. Barua zote nimezikataa. Kama kuhama ni kuhame tu."

"Kuna barua ambayo ikija utaikubali?"

"Mwanzo sikutaka barua yoyote, ila kwa sasa kuna nafasi ya mtu mmoja ambaye mpaka sasa hajaandika barua." Bishada alisema huku kimtazama Denny kwa wizi.

"Akiandika?"

"Hiyo ndiyo naisubiri."

"Nitaandika."

**ITANEDELEA JUMAMOSI**



# XAVI ATAMANI KUINOA BARCA, MESSI

**BARCELONA,** Hispania

XAVI Hernandez anakodolea macho nafasi ya ukocha Barcelona, ambapo atamnoa nyota waliyecheza naye zamani, Lionel Messi na amesisitiza yupo tayari kufanya kazi hapo Camp Nou.

Gwiji huyo wa Barca kwa muda mrefu amekuwa akihusishwa na mpango wa kuiona timu yake hiyo ya zamani na alikuwa anatajwa sana kabla ya Rais, Joan Laporta kuamua kumbakiza, Ronald Koeman.

Xavi alisaini mkataba mpya na Al Sadd Mei, mwaka huu, na kumfanya gwiji huyo mwenye umri wa miaka 41 kubakia kwa kikosi hicho cha nchini Qatari hadi mwaka 2023.

Lakini Xavi, ambaye alikuwa akishikilia rekodi ya kucheza mechi nyingi zaidi kwa Barca kabla haijavunjwa na Messi msimu huu, sasa anafikiria kuitaka kazi hiyo.

“Mara zote nipo sokoni,” alisema Xavi wakati akizungumza na waandishi wa habari Alhamisi wiki hii.

“Klabu imeamua kuendelea na Koeman na namtakia kila la heri.

“Kwa kipindi cha miezi hii minne iliyopita, sijawasiliana na (rais Laporta) au mtu mwingine yeyote kwenye bodi.

“Sijui ni wakati gani utakuja, lakini kwa upande wangu itakuwa ni ndoto nzuri kurudi tena Barca siku moja. Sina haraka sana, lakini nina matumaini itatokea.”

# Mancini: Italia itafanya makubwa Euro 2020

**ROME,** Italia

ROBERTO Mancini anajiamini kwamba, timu ya Italia itafikia nusu fainali ya michuano ya Euro 2020 iliyoanza jana.

‘Azzurri’ hao jana walifungua pazia la michuano hiyo kwa kucheza na Uturuki katika dimba la Olimpico hapo Roma.

Baada ya kukosa kufuzu michuano ya Kombe la Dunia mwaka 2018, sasa imekuwa ni miaka mitano tangu Waitaliano hao wacheze kwenye michuano mikubwa ya soka.

Lakini baada ya kuiongoza Italia kutofungwa katika mechi zake 27, inatajwa kama moja ya timu inayopewa nafasi kubwa ya kulibeba kombe hilo.


Na kocha huyo wa zamani wa Manchester City, anaimani kwamba kikosi hicho kina nafasi ya kufika nusu fainali ambayo itachezwa Uwanja wa Wembley.

“Nafikiri baada ya kila kitu tulichopitia, sasa ni wakati wa kuwa na tabasabu nzuri usoni mwetu,” alisema akiwaambia waandishi kabla ya mchezo wa jana.

“Hilo litakuwa baada ya mwezi mmoja, na tunataka watu wafurahie wenyewe uzuri wa kushabikia soka.

“Nafikiri tutakuwa wa aina yake kwa kila mmoja katika dakika zote 90, tutafanya kila kitu.”






# *Hispania ina njaa na Euro 2020 - Thiago*

**MADRID,** Hispania

THIAGO Alcantara amesema kwamba, kikosi cha Hispania kina njaa ya mafanikio kwenye michuano ya Euro 2020.

Kocha Luis Enrique atakiongoza kikosi chake kufungua dimba kwenye michuano hiyo kwa kucheza na Sweden Jumatatu katika Uwanja wa La Cartuja mjini Seville.

Kikosi hicho kilikumbwa na dhahama baada ya Sergio Busquets kukutwa na maambukizi ya virusi vya corona pamoja na Diego Llorente kabla ya mchezo wa kirafiki dhidi ya Lithuania, Jumanne.

Na Thiago, kiungo wa Liverpool anaona kwamba kikosi hicho kina njaa kali ya kupata mafanikio kwenye mashindano hayo licha ya baadhi ya wachezaji wake kukumbwa na maambuziki ya virusi vya corona.

Aliliambia Marca: “Soka limebadilika. Licha ya vipaji timu itakayokuwa imejiandaa vizuri itashinda kwa ubora.

“Tunazungumza kuhusu wachezaji bora Ulaya na mashindano bora kabisa.

“Tuna timu yenye vijana wengi na tupo tayari kwa mashindano haya na vijana wana njaa kubwa ya kufanikiwa.”

## HABARI MICHEZO

# Deschamps hafikirii kuitosa Ufaransa

**PARIS,** Ufaransa

DIDIER Deschamps amebainisha kwamba, ataendelea kuwa kocha wa Ufaransa hata baada ya mkataba wake wa sasa kumalizika, ambao umebaki mwaka mmoja.

Deschamps aliiongoza Ufaransa kwenye fainali ya michuano ya Euro 2016 na kushinda Kombe la Dunia mwaka 2018 akiwa na 'Les Bleus' hao.

Yeye ni kocha wa tatu baada ya Mario Zagallo na Franz Beckenbauer – ambao wameshinda Kombe la Dunia wakiwa wachezaji na makocha, huku pia akitarajiwa kuweka historia mpya kama ataiongoza Ufaransa kushinda Euro 2020 mwaka huu.

Ufaransa ilitinga fainali ya michuano hiyo wakati ilipocheza kwenye ardhi yake mwaka 2016, na kama Deschamps atabeba taji hilo mwaka huu atakuwa mtu wa kwanza kushinda Euro na Kombe la Dunia kama mchezaji na kocha.

Hata hivyo, michuano hiyo inaweza kuwa ya mwisho kwake kuongoza Ufaransa, kwani mkataba wake wa sasa unamalizika mwishoni mwa mwaka 2022, baada ya Kombe la Dunia nchini Qatar.

Lakini Deschamps, hana mpango wa kuondoka kwenye nafasi hiyo, hasa kwa sababu anaungwa mkono na Shirikisho la Soka la Ufaransa, FFF.

"Naweza kuendelea baada ya mwaka 2022 kwa makubaliano na rais," alisema Deschamps akiiambia RTL.

"Watu wanataka mimi nibaki na matokeo ndio yanayohitajika. Nitafanya kitu fulani, lakini ningependa kuendelea kuwapo."





# ZIYECH HANA CHAKE CHELSEA

**LONDON,** England

KLABU ya Chelsea imesema ipo tayari kumuuza kiungo wake, Hakim Ziyech kwenye usajili wa msimu ujao, licha ya kukaa kwa msimu mmoja tu.

Ziyech anaelezwa kushindwa kukidhi matarajio ya Chelsea katika msimu huu wa kwanza kwani hakuwa kwenye kikosi cha kwanza cha makocha aliofanya nao kazi, Frank Lampard na Thomas Tuchel.

Chelsea ndiyo ilishinda mbio za kumnasa Ziyech kutoka Ajax Amsterdam ya Uholanzi baada ya kuonyesha kiwango kizuri kwa misimu kadhaa mfululizo na klabu nyingi za Ulaya kuwania saini yake zikiwamo Manchester United, Real Madrid, Barcelona na Bayern.

Taarifa zinasema klabu za Italia, Napoli na AC Milan zimeweka wazi kumhitaji mchezaji huyo raia wa Morocco ili kuongeza nguvu kwenye vikosi vyao kwa msimu ujao na zipo tayari kwa dau lolote.

Takwimu za Ziyech akiwa Chelsea msimu huu wa 2020-2021, zinaonyesha amecheza mechi 23 za Ligi Kuu England na kufunga mabao mawili na mechi 16 za mashindano mengine ikiwamo Ligi ya Mabingwa Ulaya ambapo amefanikiwa kufunga kucheka na nyavu mara nne, hivyo amefunga mabao sita katika michezo 39.

# Bilionea atoa ofa kuinunua Arsenal

**LONDON,** England.

BILIONEA wa Spotify, Daniel Ek, ameongeza dau katika mpango wake wa kutaka kuinunua Arsenal, na sasa ameweka mezani pauni bilioni mbili.

Ek, ambaye ni shabiki wa Arsenal ofa yake ya mwanzo ya kununua timu hiyo ilikwama na sasa tajiri huyo raia wa Sweden, amekuja na ofa ya pili na anaamini inaweza kumshawishi mmiliki wa klabu hiyo ya Emirates, Stan Kroenke kufanya biashara.

Ofa yake ya kwanza ya pauni bilioni 1.8 ilikataliwa mwezi uliopita, kabla ya sasa kuongeza pauni milioni 200.

Katika ofa yake ya mwanzo, Ek alisema kitu ambacho alijibiwa na wamiliki wa Arsenal wa sasa, Mmarekani Kroenke ni kwamba hawana shida ya pesa, lakini anaamini kwa kupandisha dau zaidi linaweza kufanya mchakato huo ukakubalika.

Kambi ya bilionea Ek, ilisema "hatuendi kokote hadi hapo tutakapoona hili dili limekamilika."

Watu wa ndani wa klabu ya Arsenal wamekiri wanatarajia kupokea ofa ya pili ya kuhusu mpango wa kuinunua timu hiyo kwa mujibu wa Daily Mail.

Ek anajaribu kutumia mwanya wa michuano ya European Super League ambayo imewafanya mashabiki wa Arsenal kuwachukia wamiliki wa klabu hiyo kwa sasa ili kufanikisha mpango wake wa kuibeba jumla timu hiyo.



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# MAN UNITED WAGONGA MWAMBA KWA SANCHO

●●● Hudson Odoi, Dembele, Ronaldo sasa waendelea kutajwa baada ya...

**MANCHESTER,** England

OFA ya kwanza ya Manchester United kwa ajili ya kumsajili Jadon Sancho, imekataliwa na Borussia Dortmund, kwa mujibu wa BBC Sport.

**Man United imekuwa ikimuwania kwa muda mrefu Sancho ambaye ni mchezaji wa timu ya Taifa ya England mwenye umri wa miaka 22.**

Na mapema juzi Man United ilitoa ofa ya awali ya pauni milioni 67 kwa ajili ya kumsajili winga huyo, lakini ilikataliwa na miamba hao wa Ligi Kuu Ujerumani, Bundelsiga.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, Dortmund bado wameshikilia msimamo wa kutaka angalau pauni milioni 77.5 ili kuwa tayari kumuachia mchezaji huyo.

Mapema Januari mwaka huu, United walikaribia kumsajili Sancho, lakini dili hilo likafa katika dakika za mwisho.

Na kipindi hiki cha usajili wa majira ya joto, Man United walikuwa na uhakika wa kumsajili nyota huyo kwa ajili ya kuimarisha kikosi chao tayari kwa msimu mpya wa 2021-2022.

Hata hivyo, kikosi hichyo cha kocha Ole Gunnar Solskjaer, sasa kitatakiwa kuongeza dau ili kufikia kiwango kinachotakiwa na Dortmund kuruhusiwa kumsajili nyota huyo.

Taarifa zaidi kutoka pale Ol Trafford zinaeleza kuwa, iwapo mazungumzo mengine ya kumsajili Sancho yatagonga mwamba, Man United huenda ikawawinda nyota wengine kuziba pengo la winga huyo.

Nyota wanaotajwa sasa kuwaniwa na Man United ni pamoja na Hudson Odoi, Ousmane Dembele na nyota wa Juventus, Christiano Ronaldo.

## ZISIKUPITE

### CHELSEA YAKOMAA NA HAKIMI

CHELSE inataka kumsajili beki wa kulia wa Inter Milan na Morocco, Achraf Hakimi, 22. Mchezaji huyo amekuwa akinyatiwa pia na klabu ya PSG. ***(Times)***

### ODOI MTEGONI CHELSEA

IWAPO Chelsea itamsajili Achraf Hakimi, inaweza kusikiliza ofa za kumuuza winga wa England, Hudson Odoi, 20 au Tino Livramento, huku Aston Villa ikiwa na hamu ya kumsajili beki huyo wa kulia. ***(Guardian)***

### PSG YAMUWINDA DEMBELE

KLABU ya Paris St-Germain inachunguza hali ya mshambuliaji wa Ufaransa, Ousmane Dembele, 24, ambaye mkataba wake na Barcelona umesalia mwaka mmoja kumalizika. ***(Marca)***

### STERLING ATAJWA BARCA

BARCELONA inafikiria kumsajili nyota wa England na Manchester City, Raheem Sterling, ambaye anaonekana kama chaguo lao kuchukua nafasi yake Ousmane Dembele kama hataongeza mkataba wake.

### MESSI ATAKIWA MAREKANI

MMILIKI wa Inter Miami, Jorge Mas, amethibitisha kwamba yeye na mmiliki mwenza wa klabu hiyo, David Beckham wamekuwa na mazungumzo na Lionel Messi, 33. ***(Miami Herald)***

### NEYMA AMLILIA MBAPPE PSG

NYOTA wa Brazil, Neymar 29, aliweka sharti aliposaini mkataba mpya na PSG kwamba hawatamuuza mshambuliaji wa Ufaransa, Kylian Mbappe, 22, msimu huu. ***(AS)***

### SPURS YAMTAKA THURAM

KLABU ya Tottenham Hotspur wanafanya mazungumzo na winga wa Borussia Monchengladbach, Marcus Thuram, 19, kwa ajili ya kumsajili. Thuram ni mtoto wa mshindi wa Kombe la Dunia na Ufaransa mwaka 1998, Lillian. ***(RMC Sport)***

### WINKS ANATAKIWA SPURS

MKURUGENZI wa michezo wa Tottenham, Fabio Paratici, amesema wanafikiria kumsajili, Harry Winks, 25. ***(Football Insider)***

### XHAKA MALI YA ROMA

AS Roma wanakaribia kukamilisha taratibu za kumsajili kiungo wa kati wa Arsenal, Granit Xhaka, 28. ***(Corriere dello Sport)***

### SABITZER KUONDOKA

KIUNGO wa RB Leipzig, Marcel Sabitzer, 27, anataka kuondoka katika klabu hiyo ya Bundesliga. ***(Athletic)***

### LAMPARD ATAJWA PALACE

KOCHA wa zamani wa Chelsea, Frank Lampard, amerejea kazini, lakini safari hii katika klabu ya Crystal Palace baada ya mazungumzo na kocha wa zamani wa Wolves Nuno Espirito Santo, kugonga mwamba. ***(Mirror)***

**HABARI MICHEZO**

# Watunisha misuli kushindana Oktoba

**Na Shufaa Lyimo**

MASHINDANO ya kutunisha misuli kwa wanaume na wanawake, yanatarajiwa kufanyika Oktoba 15, mwaka huu jijini Dar es Salaam, imeelezwa.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam wiki hii, Mwenyekiti wa Kamati ya mashindano hayo, Nilesh Batt, alisema yatafanyika kwa mara ya nane tangu kuanzishwa kwa shirikisho la mchezo huo hapa nchini.

Mwenyekiti huyo alisema kabla ya kuanza kwa mashindano hayo wataandaa semina kwa ajili ya kuwapiga msasa majaji wote ambao watasimamia ili waweze kufahamu kanuni ya mchezo huo, ambao umesaidia vijana wengi kupata ajira.

"Maandalizi kwa ajili ya mashindano hayo yanaendelea vizuri, kadhalika kutakuwa na zawadi ambazo zitatolewa kwa washindi wote, hivyo tunaomba Watanzania kujitokeza kwa wingi siku hiyo ili kushuhudia vipaji vitakavyoonyeshwa na washiriki wetu," alisema Nelish.

Alizitaja zawadi zitakazotolewa kuwa, mshindi wa kwanza kwa kwa wanaume (Mr. Tanzania), ataibuka na Sh. milioni tano na kwa upande wa wanawake (Miss Fitness General) akizawadiwa Sh.milioni tatu.

Katibu Mkuu wa shirikisho hilo (TBBF), Francis Mapugilo, alisema washiriki watakaoshiriki kinyang'amyiro hicho ni wale wenye miili ambayo misuli yao inaonekana kutuna zaidi, huku akifafanua kwamba kupitia mchezo huo wamefanikiwa kutoa washiriki kwenda kushindana nje ya nchi na kurudi nyumbani wakiwa na medali za ushindi.

"Oktoba 12, tutafanya mchujo wa washiriki na kubaki na wale ambao watakuwa wamekidhi vigezo vya mashindano, lengo ni kuwa na timu bora," alisema.



# MULTICHOICE YATANGAZA MAFUNZO UANDAAJI FILAMU

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya MultiChoice kwa kushirikiana na Bodi ya Filamu Tanzania, imetangaza rasmi fursa ya mafunzo ya uandaaji wa filamu kwa vijana wa Kitanzania kupitia programu maalum inayojulikana kama MultiChoice Talent Factory.

**Programu hii ilizinduliwa rasmi Mei 2018 na imekuwa ikitoa mafunzo maalum ya uzalishaji filamu katika akademi maalum za MultiChoice Talent Factory Academy.**

Akizungumza wakati wa ufunguzi rasmi wa kupokea maombi kwa awamu ya tatu, Mkuu wa Uhusiano MultiChoice Tanzania, Johnson Mshana, alieleza kuwa programu hiyo ni muendelezo wa programu maalum iliyodhamiria kuleta mabadiliko katika tasnia ya filamu barani Afrika.

"Baada ya miaka miwili ya mafanikio, MultiChoice inajivunia kutangaza awamu nyingine ya mafunzo ya uandaaji wa filamu kwa vijana wa Kitanzania wenye wito na masuala ya filamu.

"Tulianza kwa kupeleka vijana wanne katika akademi maalum kule Nairobi nchini Kenya Oktoba 2018, kisha vijana wengine wanne Oktoba 2019 ambao walihitimu mafunzo yao Aprili mwaka huu, na leo tunafungua rasmi dirisha la kupokea maombi kwa vijana wengine wa Kitanzania wenye wito na kazi za filamu kwa ajili ya darasa la mwaka 2022.

Maombi yote yatapokelewa kwa njia ya mtandao kupitia tovuti yetu ya https://cte.multichoicetalentfactory.com/Home/MTFHome. Na mchakato wa usajili utafanyika Julai hadi Agosti, mwaka huu na majina ya vijana watakaokidhi vigezo yatatangazwa mara baada ya mchakato kumilika ama kwa msaada zaidi namna ya kujiunga wasiliana na grace.mgaya@mutichoice.co.tz au simu namba 0765 065300," alisema Mshana.

Kwa upande wa Katibu Mtendaji wa Bodi ya Filamu Tanzania, Dk. Kiagho Kilonzo, kwanza alipongeza Kampuni ya MultiChoice kwa kuwa mstari wa mbele katika kuleta mapinduzi kwenye tasnia ya filamu hapa nyumbani Tanzania.

"Binafsi ni shuhuda wa jitihada zinazofanywa na Kampuni ya MultiChoice katika kuhakikisha kwa pamoja tunaipeleka mbele tasnia hii na kufika katika viwango vya kimataifa.

"Hakika hii ni fursa ya kipekee kwa vijana wetu na ninapenda kuchukua nafasi hii kuwahamasisha vijana wote wenye wito na masuala ya filamu na sanaa kwa ujumla kuitumia nafasi hii ipasavyo ili kuweza kujifunza, kubadilishana ujuzi na hatimaye siku zijazo nchi yetu iweze kupata waandaji wa kazi zenye maudhui ya hali ya juu," alisema Dk. Kilonzo



Ofisa Uhusiano wa MultiChoice Tanzania, Grace Mgaya, akitoa ufafanuzi wa namna ya kutuma maombi ili kupata udhamini wa mafunzo ya uandaaji filamu yanayotolewa na Kampuni ya MultiChoice kupitia programu ya MultiChoice Talent Factory, jana Kivukoni, Dar es Salaam. Katikati ni Katibu Mtendaji wa Bodi ya Filamu Tanzania, Dk. Kiagho Kilonzo na kushoto ni Emmanuel Ndumukwa, Mkurugenzi wa Maendeleo ya Kazi za Filamu nchini. **NA MPIGAPICHA WETU**

# *Manyama tayari Azam FC, sasa yageukia 'mapro'*

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

BAADA ya kuweka wazi usajili wa beki wa kushoto kutoka Ruvu Shooting, Edward Manyama, uongozi wa Azam FC umesema mchakato wa kuimarisha kikosi chao unaendelea, huku sasa ikitajwa kuwania saini ya mlinzi wa kulia wa Coastal Union, Hassan Kibailo.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Mtendaji Mkuu wa Azam FC, Abdulkarim Amin 'Popat', alisema wamekamilisha usajili wa Manyana kwa mkataba wa miaka mitatu kukitumikia kikosi cha timu hiyo kuanzia msimu ujao.

Alisema usajili wa nyota huyo ni mapendekezo ya ripoti waliyokabidhiwa na kocha George Lwandamina kuelekea maboresho anayotaka kuyafanya katika baadhi ya nafasi.

"Tumemalizana na Manyama kwa kufuata kanuni zote za usajili baada ya huyo, tunaendelea na mchakato wa usajili kwa wachezaji wa kigeni kwa nafasi alizozihitaji kwa lengo la kuimarisha kikosi chetu kwa msimu ujao.

"Kuhusu wachezaji wa kigeni, tayari mchakato unaendelea na tunahitaji kuwa na kikosi bora zaidi ili kufanya vizuri katika michuano inayotukabili kwa msimu ujao ikiwamo Ligi Kuu na michuano ya kimataifa; Kombe la Shirikisho barani Afrika," alisema Popat.

Hata hivyo, Azam imeonekana kutaka kuimarisha beki wa kulia na kushoto kwa kusajili mabeki wa Kitanzania kuwasaidia Mzimbabwe Bruce Kangwa na Mganda Nicolaus Wadada.

Kuhusu Kibailo kuwindwa na Azam FC, beki huyo alimwambia mwandishi wetu kuwa ni kweli mkataba wake na Coastal Union unaisha mwisho mwa msimu huu na kuna timu nyingi zinamhitaji, lakini hakuitaja moja kwa moja Azam FC.

"Ni kweli mkataba wangu na Coastal unaisha mwisho wa msimu huu na kuna timu nyingi zinanihitaji na zimewasiliana na mimi, lakini bado nipo na viongozi wangu wa Coastal kama wanaweza kunifanya nibaki au vipi," alisema beki huyo.

# Michezo

Jumamosi Juni 12, 2021

Nipashe




## Man Utd wagonga mwamba kwa Sancho

UKURASA 22



INJINIA...

Kiungo wa Klabu ya Simba na timu ya Taifa ya Uganda, Injinia Taddeo Lwanga (juu), akikutana na kigingi kutoka winga wa kulia wa timu ya Taifa ya Afrika Kusini (Bafanabafana), Denwin Farmer, wakati wa mechi ya kimataifa ya kirafiki iliyopigwa Uwanja wa Orlando, Afrika Kusini juzi na kumaliza kwa Waganda hao kulala kwa mabao 3-2. **PICHA: MTANDAO**

## Simba, Yanga SC wafungukia suluhu

**Na Adam Fungamwango**

MAKOCHA wa timu za Simba na Yanga chini ya miaka 20, wamefunguka kuhusu suluhu waliyopata juzi usiku katika Uwanja wa Azam Complex kwenye mechi ya Kundi A ya Ligi ya Vijana Tanzania Bara kwa umri huo.

Wakati Kocha Mkuu wa Yanga, Said Maulidi, akisema kuna wakati wachezaji wake walikuwa wakiingia mchecheto kutokana na mekelele ya mashabiki nje ya uwanja, Kocha Mkuu wa Simba, Nico Kiondo, amesema timu yake ingeweza kuibuka na ushindi kama vijana wake wangetumia vizuri nafasi chache walizopata.

"Ndiyo, sisi tulikuwa tunatumia mashambulizi ya kushtukiza na ni kweli wenzetu walikaa sana na mpira, lakini hiyo haikuwa sababu ya kutoka suluhu nao ya bila kufungana. Nilitengeneza mkakati niwafunge ili nipate ubingwa, lakini kwa bahati tumetoka sare. Kuna wakati ilibidi nipige kelele sana kwa sababu niliona wachezaji wangu wanapotea, hasa mabeki. Makelele ya mashabiki nje yalionekana kuwachanganya sana, unajua hawa ni vijana na si mara kwa mara wanakutana na mashabiki wengi vile," alisema winga huyo wa zamani wa Yanga.

Naye kiungo wa zamani wa Simba, Kiondo, yeye alisema walimiliki kwa kiasi kikubwa mpira, lakini vijana wake hawakutumia nafasi chache walizozipata.

"Yanga hawakunizidi, wao walifanya mashambulizi ya kushtukiza tu, lakini mimi nilitawala mchezo, ila vijana wangu hawakuwa makini kumalizia nafasi," alisema.

Katika mechi nyingine ya Kundi hilo la A, JKT Tanzania iliibuka na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Mwadui FC, hivyo kukaa kileleni ikiziacha Simba na Yanga zikishika nafasi ya pili.

# Mtifuano mkali uchaguzi TFF

**Na Mwandishi Wetu**

### Tisa wamvaa Karia, Hawa awa mwanamke pekee kutaka kumng'oa, Wakili Kibamba afunguka...

ZIKIWA zimebaki saa chache kabla ya dirisha la kuchukua na kurejesha fomu za kuwania uongozi wa juu wa Shirikisho la Soka nchini (TFF) kufungwa leo saa 10:00 alasiri, mtifuano huo umezidi kuwa mgumu baada ya jumla ya wagombea tisa kujitokeza kuchukua fomu wakiwa na lengo la kukitaka kiti cha Rais anayetetea nafasi yake, Wallace Karia.

**Jana waliongezeka wagombea watatu waliochukua fomu za kuwania kiti cha urais wa shirikisho hilo katika Ofisi za TFF na kufanya jumla sasa kuwa 10 pamoja na Karia, ambao ni mwandishi, mchambuzi na wakala wa wachezaji, Ally Saleh kutoka Zanzibar, Rahim Kangezi na mwanadada pekee, Hawa Mniga.**

Hivyo sasa wanaungana na Mwenyekiti wa zamani wa Yanga na Mbunge wa Kinondoni (CCM), Abbas Tarimba, kiungo wa zamani wa Yanga, Ally Mayay Tembele, Deogratius Mutungi, Evans G. Mgeusa, mwandishi na mchambuzi wa soka, Oscar Oscar na Mbunge wa Jimbo la Mwera mjini Zanzibar, Zahor Mohammed Haji.

Kwa upande wa nafasi ya Kamati ya Utendaji kwa Kanda namba 1- Dar es Salaam, Lindi, Morogoro, Mtwara na Pwani waliochukua fomu ni wagombea nane ambao ni Lameck Nyambaya, Liston Katabazi, Michael Petro, Saady Mohamed Kimji, Athuman Kingome Kambi, Elyson Mweladzi, Michael Petro na Muharam Mazoka.

Kanda namba 2- Arusha, Kilimanjaro, Manyara na Tanga ni Khalid Abdallah na Zakayo Mjema huku Abousufian Sillia, James Mhagama na Joseph Ngunangwa wakichukua fomu kwa Kanda namba 3- Iringa, Mbeya, Njombe, Ruvuma na Songea.

Kwa upande wa Kanda namba 4 - Dodoma, Shinyanga, Simiyu na Singida walijitokeza kuchukua fomu ni Mohamed Aden, Osuri Kosuri na Hamisi Juma Kitilia wakati Kanda namba 5- Geita, Kagera na Mwanza ni Salum Umande Chama na Vedatus Lufano na kwa Kanda namba 6- Katavi, Kigoma, Rukwa na Tabora ni Blassy M. Kiondo na Issa Mrisho Bukuku.

Aidha, Mwenyekiti wa Kamati ya Uchaguzi ya TFF, Wakili Kiomoni Kibamba, jana alimwambia mwandishi wetu kuwa mwitiko wa wagombea hasa nafasi ya urais ni mzuri, hivyo anatoa wito kwa wanafamilia wenye nia ya kugombea kutumia siku moja iliyobaki (leo) kuchukua na kurejesha fomu hizo.

"Yapo maoni mengi kutoka kwa Watanzania kuhusu mchakato wa uchaguzi unaoendelea hivi sasa. Ushauri wetu kwao ni kuendelea kufuatilia, kwa vile mchakato unaendeshwa kwa kuzingatia miongozo iliyopo ambayo ni Katiba ya TFF pamoja na Kanuni za Uchaguzi wa TFF," alisema.

Kuhusu wagombea waliowaandikia kuomba mwongozo au kuwapa mapendekezo yao kuhusiana na uchaguzi huo, Kibamba alisema wamewapa majibu kwa maandishi.

Alisema mbali ya kuendesha mchakato huo, moja ya majukumu ya kamati hiyo baada ya uchaguzi ni kutoa tathmini nzima na mapendekezo kama yatakuwapo kwa mamlaka zenye nguvu ya kurekebisha katiba, sheria, kanuni pamoja na taratibu.

"Kama taratibu zilivyo, Katiba au Kanuni za uchaguzi haziwezi kufanyiwa marekebisho wakati mchakato unaendelea," alisema Wakili Kibamba.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >